# Umeme wafikishwa JNHPP majaribio ya uzalishaji




Uk. 3

# Vyakula vinne bora kwa kuboresha kumbukumbu



Uk. 14



Uk.23

*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

# Uelekeo



# Mwinyi na kimbunga cha maendeleo Zanzibar

Uk. 12

| ISSN 2953-2787 | Toleo Na. 00046 | Bei Tanzania sh 1,000 | Jumatano Januari 10 - 16, 2024 |



Uk. 2

## 18 waugua kipindupindu Shinyanga



## Maporomoko Hanang yaua wanafunzi 22

Uk. 3



## SMZ mbioni kukamilisha madarasa 5,000

Uk. 3

# Dk. Samia: Chapa ya karafuu Z'bar ilindwe

- **Aagiza kilimo cha mkataba kwa mashamba ya serikali**



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, akifungua Jengo la Kitega Uchumi la Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC), kisiwani Pemba jana, ikiwa ni moja na shamrashamra za miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

## TPA yatenganisha utekelezaji wa miradi





Uk. 2

## Mume adaiwa kumchinja mkewe, kutenganisha kichwa na kiwiliwili

Uk. 4

# 18 waugua kipindupindu Shinyanga

**Na Mwandishi Wetu, Shinyanga**

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, amesema watu 18 kati ya 41 ambao walikabiliwa na tatizo la kuhara na kutapika, wamebainika kuwa na ugonjwa wa kipindupindu mkoani hapa.

Desemba 28, mwaka jana, Mkoa wa Shinyanga katika Kata ya Kagongwa wilayani Kahama, kulitokea vifo vya watu watano ambao walikabiliwa na ugonjwa wa kuhara na kutapika na kusababisha Mkoa kuunda timu ya wataalamu kufuatilia tatizo hilo. Mndeme akizungumza jana na waandishi wa habari, alisema awali vifo vya watu hao havikubainika moja kwa moja kwamba vilisababishwa na kipindupindu.

Alisema katika wagonjwa wengine 41 ambao nao pia walikuwa wakikabiliwa na ugonjwa huo wa kuhara na kutapika, baada ya kupata vipimo, 18 walibainika kuwa na kipindupindu na walipatiwa matibabu, hadi sasa wamesalia wagonjwa watano wakiendelea na matibabu.

"Wagonjwa hawa 18 ambao walibainika kuwa na kipindupindu, 15 wanatoka Kahama, wawili wanatoka katika Manispaa ya Shinyanga na mmoja anatoka Kishapu Natoa wito kwa wananchi wazingatie masuala ya usafi hasa kipindi hiki cha msimu wa mvua," alisema.



# TPA yatenganisha utekelezaji wa miradi



**Tumeona haja ya kuharakisha ujenzi wa bandari ya Bagamoyo kutokana na hali iliyopo...**



**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), imeamua kutenganisha utekelezaji wa mradi wa ujenzi Bandari Bagamoyo na mradi wa Eneo Maalumu la Kiuchumi Bagamoyo.

Awali, ilielezwa ujenzi wa mradi wa Bandari ya Bagamoyo utahusisha pia ujenzi wa mradi wa eneo maalum la kiuchumi.

Hayo yalielezwa jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Plasduce Mbossa, alipozungumza na waandishi wa habari jana.

"Tunaanzia na gati mbili ndefu na hizo zitajengwa na sisi TPA, baadaye zinazofuata na tupo tayari kupokea mwekezaji kutoka sekta binafsi atakayejenga kwa kushirikiana na serikali," alisema.

Aidha, aliongeza kuwa awali mpango ulikuwa ujenzi wa mradi huo uhusishe na ujenzi wa eneo maalumu la uchumi lakini wameamua kutekeleza miradi hiyo kwa nyakati tofauti.

"Tumeona haja ya kuharakisha ujenzi wa bandari ya Bagamoyo kutokana na hali iliyopo, kwamba baadhi ya meli haziwezi kuhudumiwa na Bandari ya Dar es Salaam kutokana na magati kuwa mdogo," alisema.

Hata hivyo, Mbossa alisema wanatarajia mradi huo kukamilika mwaka 2028 na kwa sasa mchakato wa kumpata mzabuni unaendelea.

# Atupwa jela maisha kwa kunajisi

**Na Mwandishi Wetu, Pwani**

MKAZI wa Kibaha mkoani wa Pwani, Said Sadick Said (23), amehukumiwa kwenda jela maisha, baada ya kukutwa na hatia ya kumnajisi mwanafunzi mwenye umri wa miaka minane wa shule ya msingi iliyopo Halmashauri ya Mji wa Kibaha.

Hukumu hiyo ilitolewa juzi na Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Kibaha, Fahamu Kibona, baada ya mahakama hiyo kuridhika na ushahidi uliotolewa wakati wa usikilizwaji wa kesi hiyo namba 66 ya mwaka 2023.

Kabla ya kutoa hukumu hiyo, mahakama ilimpa mshtakiwa nafasi ya kujitetea kwanini asipewe adhabu kali, ambapo alidai hajui kama ana kesi na pia hajui chochote kuhusu kesi hiyo.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Kibona alisema mtuhumiwa alitenda kosa hilo kwa nyakati tofauti kuanzia Januari hadi Septemba, mwaka jana eneo la Mpiji- Kibaha na kwamba kwa mujibu wa sheria, anapaswa kwenda jela maisha.

Alisema mama mzazi wa mwanafunzi ndiye aligundua jambo hilo baada ya kukuta haja kubwa kwenye moja ya nguo za ndani za mwanafunzi huyo na akamuuliza kuhusiana na hali hiyo.

"Baada ya mama mzazi kukuta haja kubwa kwenye nguo ya mwanafunzi huyo, alimuuliza kuhusu hali hiyo awali alikanusha na baadaye alimueleza mama yake kuwa hiyo imetokana na kunajisiwa na muuza maziwa na kutaja jina," alisema.

Alisema mwanafunzi huyo alisema siku ya kwanza mtuhumiwa alikutana na mwanafunzi huyo aliyekuwa akielekea kwa rafiki yake, ambapo alimshika mkono na kumvutia chini ya mwembe kisha kuanza kumnajisi na alipofanikisha unyama huo alimtishia kuwa asiseme kwa mtu yeyote.

Kwa mujibu wa hakimu huyo, upande wa mashitaka uliwasilisha mashahidi watano ambao ni mwanafunzi aliyeathirika na kitendo hicho, mama wa mwanafunzi huyo, mpelelezi wa kesi, daktari na askari aliyemkamata mtuhumiwa.

Hakimu Kibona alieleza kuwa wakati wa usikilizwaji wa kesi hiyo, upande wa Jamhuri uliwakilishwa na mawakili wawili ambao ni Elizabeth Olomi, akisaidiana na Neema Kwayi.

Wakizungumza nje ya mahakama, baadhi ya wakazi mkoani humo walisema hukumu hiyo itaongeza woga kwa baadhi ya watu wenye tabia hiyo, kwa kuwa kitendo hicho kinaathiri watoto ambao ndiyo nguvu kazi ya Taifa kwa miaka ijayo.

"Kama ni kweli alitenda kosa hilo, mwache aende ni haki yake naamini wengine watajifunza kupitia kwake," alisema mmoja wa wakazi wa Kibaha.

# Maporomoko Hanang yaua wanafunzi 22

**Na Mwandishi Wetu, Manyara**



MKUU wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, amesema wanafunzi 22 wamefariki dunia kufuatia ya maporomoko ya matope kutoka Mlima Hanang' Desemba 3, mwaka jana.

Alisema 15 kati yao, wanatoka Shule ya Msingi Jordom.

Mkuu huyo wa mkoa, alisema hayo jana wakati akitoa taarifa ya wanafunzi kurejea shuleni baada ya shule kufunguliwa ikiwa ni muhula mpya wa masomo kwa mwaka 2024.

Kwa upande wake Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Jordom, Balitoga Mpanula, alisema shule hiyo ilipoteza wanafunzi 15 katika tukio la maporoko kutoka Mlima Hanang' na kwa sasa Serikali imeendelea kuwahudumia manusura wa tukio hilo kwa kuwapatia vifaa vya shule.

Kwa upande wake, Mkuu wa Shule ya Sekondari Ganana A, Sophia Maley, akitoa taarifa ya kuripoti kwa wanafunzi kwa mwaka mpya wa 2024, alisema shule hiyo imepoteza wanafunzi wawili kufuatia maporomoko hayo wakati mmoja alijeruhiwa na hali yake sasa inaendelea vizuri.

# SMZ mbioni kukamilisha madarasa 5,000

**Na Mwandishi Wetu, Zanzibar**

RAIS wa Zanzibar ambaye pia ni Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema Serikali inakaribia kumaliza ujenzi wa madarasa 5,000 kuondoa zamu mbili kwa wanafunzi nchi nzima na kubakisha zamu moja.

Aliyasema
hayo jana alipofungua rasmi Skuli mpya ya Sekondari Tumekuja iliyopo Mwembeladu Wilaya ya Mjini Mkoa wa Mjini Magharibi katika shamrashamra za miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Vilevile, skuli hiyo ina uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,755 kwa wastani wa uwiano wa wanafunzi 45 kwa darasa moja na tayari wameshapangwa wiki ijayo kuanza masomo.

Rais Dk. Mwinyi alimpongeza mkandarasi wa kampuni ya CRJE kwa kujenga skuli ya kisasa ambayo ina maabara tatu, chumba cha kompyuta, maktaba na ukumbi wa mikutano.

Alisema Serikali itaendelea kujenga maghorofa katika sekta ya elimu kwa wanafunzi kutozidi 45 kwa darasa moja.

Hali kadhalika, alisema Serikali itaendelea kufanya uamuzi sahihi kwa faida ya nchi na kuyakarabati majengo ya Mji Mkongwe kwa kuwa ni urithi wa nchi kwa manufaa ya vizazi vijavyo.

Kwa upande mwingine, Rais Dk. Mwinyi alisema mafanikio yaliyopatikana katika elimu ni kwa juhudi za walimu kwa kuongeza idadi ya ufaulu ikiwemo kutoka wanafunzi 2,000 hadi 6,000 kwa skuli za msingi na matokeo ya kidato cha sita ya mwisho ufaulu wa daraja la kwanza hadi daraja la tatu kwa asilimia 90.



Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi.

# Jafo atoa siku 7 wamiliki mgodi kufika NEMC



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo.

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, ametoa sikusaba kwa wamiliki wa mgodi wa madini ya kaorini uliopo Kimani kwenda ofisi za NEMC kutoa maelezo.

Jafo alitembelea mgodi huo ambapo hakuridhishwa na shughuli za uchimbaji wa madini hayo (dongo jasi).

Akizungumza wakati wa kukagua shughuli za uchimbaji katika mgodi huo, alisema hakuridhishwa na shughuli nzima za uendeshaji ikiwemo karakana na malalamiko ya wafanyakazi kuhusu maslahi yao.

"Nikiwa kama Waziri, lakini pia Mbunge, napokea malalamiko mengi ikiwemo wafanyakazi kukatwa faini kunakotokana na maagizo ya bosi kusema dereva ajaze mzigo mwingi na kukatwa faini barabarani alisisitiza kwa Mkuu wa Wilaya Kisarawe.

"Malalamiko katika huu mgodi, yamekuwa mengi mno hata kama tunawataka wawekezaji, lakini lazima wafuate sheria na kanuni za nchi katika utekelezaji wa shughuli zao," alisema.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya Kisarawe, Fatma Nyangasa, alimhakikishia, Dk. Jafo kuwaamepokea maagizo yote ya kukutana na wafanyakazi wa mgodi huo na kusikiliza kero zao ili kukakikisha pande zote zinapata maelewano mazuri kuendelea na shughuli za uzalishaji mali na taifa kupata faida.

"Tunaomba sana kila mmoja afuate taratibu na kila mwenye changamoto, afike ofisini kwa utatuzi, zaidi nitoe wito kila mmoja apaze sauti kwa kushirikishana ili mambo yaende,"alisisitiza.

# Umeme wafikishwa JNHPP majaribio ya uzalishaji

**Na Mwandishi Wetu**

KAZI ya kusafirisha umeme kutoka kituo cha Chalinze hadi Bwawa la Mwalimu Julius Nyerere (JNHPP) kwa ajili ya majaribio ya mitambo iliyofanyika juzi, imefanikiwa.

Mratibu wa mradi huo, Mhandisi John Skauki, alisema umeme wa kilovoti 400 kutoka Chalinze, uliwasili katika kituo cha kupokea umeme kilichopo kwenye bwawa hilo kwa ajili kusaidia majaribio ya uzalishaji umeme.

Akizungumza wakati wakiendelea na kazi ya kuunganisha umeme huo, Mhandisi Skauki alisema umeme utakaofuliwa kutoka bwawa hilo, utapelekwa kwenye kituo cha switchyard cha Julius Nyerere ambao utaunganika na Gridi ya Taifa.



# Dk. Samia: Chapa ya karafuu Z'bar ilindwe

## ■ Aagiza kilimo cha mkataba kwa mashamba ya Serikali

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akitoa angalizo kuhusu kulinda hadhi, ubora na chapa ya karafuu inayozalishwa Zanzibar, ameagiza mashamba ya serikali ya zao hilo yatumiwe na wakulima kwa mfumo wa mkataba.

Rais Dk. Samia aliyasema hayo jana wakati akifungua Jengo la Kitega Uchumi la Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC), Pemba ikiwa ni moja na shamrashamra za miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema karafuu visiwani humo ni sawa na madini ya almasi au dhahabu kwa kuingiza fedha nyingi za kigeni.

Alisema kwa mfano, mwaka 2022, karafuu iliingiza kiasi cha Sh. bilioni 118, sawa na asilimia 65.6 ya mauzo yote ya Zanzibar yanayouzwa nje ya nchi.

"Serikali itaendelea kutafuta masoko ya karafuu nje ya nchi, lakini tusishushe hadhi, ubora na chapa ya karafuu yetu wakati huu tunapotafuta njia za kisayansi kuongeza tija na uzalishaji wa zao hilo.

"Zanzibar imejipatia jina maarufu la 'Visiwa vya marashi ya karafuu' kwa sababu karafuu yake ina hadhi na ladha ya kipekee sana. Tuilinde 'brand' (chapa) hiyo.

"Zamani hatukujua, tulikuwa tukiuza kwa mtu mmoja au wawili ambao walikuwa wakichanganya na karafuu kutoka nchi zao ili kupata ladha ya karafuu ya Zanzibar na kwenda kuuza kwenye masoko ya dunia," alisema na kuongeza:

"Lakini sasa hivi, karafuu ya Zanzibar inakwenda yenyewe kwenye soko la kimataifa na ndiyo maana bei nayo inakuwa siyo haba, alhamdulillah, haianguki sana," alisema.

Alisema kwa kuzingatia upekee na umaarufu wa karafuu ya Zanzibar katika soko la kimataifa, kila mmoja anapaswa kuhakikisha kwamba chapa ya karafuu ya Zanzibar na umaarufu wake, unaendelea kubaki ule ule.

"Hatuna budi kuilinda kwa kuzingatia viwango vya karafuu inayouzwa nje ya nchi," aliagiza.

Kuhusu kilimo cha mkataba, Rais Dk. Samia alisema:

"Fikirieni uwezekano wa kuwa na kilimo cha mkataba… tuna mashamba mengi ya serikali, mwaka juzi mlianza kuyatambua, sasa katika mashamba ya serikali, ingieni mikataba na wakulima.

"Wapeni nyenzo wakulima wazalishe, wavune halafu mtajuana nini cha kufanya, lengo ni kuhakikisha kila shamba linazalisha vile inavyotakiwa. Tukiyatupa tu kama tulivyoyatupa huko nyuma, basi, watu wanaingia wanalima, wanavuna na wengine wanajimilikisha, hatuna mpango maalum wa mashamba ya serikali," alisema.

Alisema kufunguliwa kwa jengo hilo pamoja na mambo mengine, kutarahisisha kazi ya kupima unyevunyevu wa karafuu kwa kutumia njia za kidigitali badala ya kupima kwa mikono.

"Sasa karafuu inanunuliwa kisayansi, dhuluma ile dhidi ya wakulima ya kupanga madaraja ya karafuu kwa kukadiria na kupima kwa mikono haipo… unyevunyevu unapimwa kwa mashine na madaraja yanapangwa kutokana na vipimo vya mashinde," alisema.

Aidha, alikemea biashara ya magendo ya zao hilo akisema wanaoathirika ni wananchi wenyewe kwa kukosa huduma za maendeleo.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

# Mume adaiwa kumchinja mkewe, kutenganisha kichwa, kiwiliwili

**Na Mwandishi Wetu, Njombe**

JESHI la Polisi Wilaya ya Makete mkoani Njombe, linamshikilia Juma Kyando (36), kwa tuhuma za mauaji ya mkewe, Tumaini Luvanda (35), kwa kumchinja na kutenganisha kichwa na kiwiliwili.

Inadaiwa kuwa baada ya kumchinja, mtuhumiwa aliukata mwili huo vipande vipande na kisha kutupa baadhi ya viungo kwenye mto na vingine akivitupa jirani na nyumba yake eneo la Kabinda wilayani humo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Mahamoud Banga, alithibitisha kutokea kwa mauaji hayo na kuahidi kuwa atatolea ufafanuzi zaidi leo.

"Tukio kweli limetokea, lakini kesho (leo) nitalitolea ufafanuzi nitakapozungumza na wanahabari," alisema Kamanda Banga.

Hata hivyo, akizungumza na wananchi wilayani Makete, Mkuu wa Upelelezi Mkoa wa Njombe, Joseph Malongo, alisema jeshi hilo limepokea tukio hilo kwa masikitiko kutokana na mtuhumiwa huyo kufanya kitendo cha kikatili na kujichukulia sheria mkononi.

Alisema Jeshi la Polisi linamshikilia mtuhumiwa huyo na kwamba litahakikisha hatua za kisheria zinachuliwa dhidi yake ikiwa ni pamoja na kumfikisha mahakamani mara tu upelelezi utakapokamilika.

"Watu wanasumbuliwa na msongo wa mawazo, nawatakeni na ninawaombeni, msiyarundike matatizo yenu, mshirikishe watu pengine inaweza kusaidia," alisema.

Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Iwawa, Joseph Mbilinyi, alisema tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia Januari 8, mwaka huu katika Kijiji cha Dombwela.

Kwa mujibu wa Mbilinyi ambaye pia ni Mwenyekiti wa Mtaa wa Dombwela, alipigiwa simu na jirani yake kuwa kuna mtu anamshambulia mke wake, ndipo alipoelekea eneo la tukio na alipofika pale, alikuta mtuhumiwa kashika panga na anatisha kiasi cha kushindwa hata kumsogelea.

Alisema mtuhumiwa huyo baada ya kumkatakata mapanga mkewe ambaye kwa sasa ni marehemu, alichukua baadhi ya viungo vya mwili huo na kwenda kuvitupa mtoni.

"Baada ya kumkata mapanga, alimuweka kwenye mfuko kisha kwenda kumtupa kwenye mto, ila uwanjani jirani na nyumbani kwake, tulikuta moyo wa mtu ambao aliutoa baada ya kumuua," alisema Mbilinyi.

Naye ndugu wa mtuhumiwa wa mauaji hayo, Medrick Kyando, alisema ndugu yake hana historia ya kuwa na matatizo ya akili, hata hivyo, ameshangaa kuona amefanya tukio hilo la kikatili kwa mke wake na kusababisha sintofahamu kwa majirani.

"Ndugu yetu hana historia ya tatizo la akili, ni fundi ujenzi, alikuwa hana makundi na hata tulipopigiwa simu kuhusu tukio hilo, tulishtuka sana," alisema Kyando.

Baadhi ya majirani akiwemo Jeita Nkwama, alisema jirani yao alikuwa anaishi vizuri na mke wake na hajawahi kusikia matukio yoyote ya ajabu, lakini wameshangaa kuona ametekeleza tukio la kikatili kwa mke wake.

"Hatuwezi kujua shida ni nini na hatuamini kama kuna binadamu anaweza kutenganisha kila sehemu ya viungo vya mkewe kama mnyama," alisema.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Mahamoud Banga.

# Mchengerwa afichua umuhimu wa walimu kwa Taifa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Mohamed Mchengerwa, amesema walimu wanaofundisha kwenye shule za msingi na sekondari nchini, ni watu muhimu katika ujenzi wa msingi thabiti kwa Taifa.

Waziri Mcheengerwa aliyasema alipokuwa akifunga kikao kazi cha Makatibu Tawala Wasaidizi Elimu na Maafisa Elimu wa Halmashauri kilichofanyika Manispaa ya Morogoro.

"Kama tunataka kujenga Taifa la kizalendo la watoto wanaolipenda, wenye uchungu nalo linapotajwa kwa mabaya, wenye moyo wa kusimama na kutetea nchi yao popote, basi msingi huo unatakiwa kujengwa shuleni kuanzia madarasa ya awali na walimu wana nafasi kubwa ya kufanikisha hilo," alisema Waziri Mchengerwa.

Aliongeza kuwa walimu ni watu muhimu kwa kuwa wana uwezo wa kujenga na kubomoa Taifa kwa kuwa wazazi wamewaamini na kuwapelekea watoto wao shuleni.

"Ninyi mnakaa nao watoto wetu kwa muda mrefu kuliko sisi wazazi. Niwatake mkawafundishe uzalendo, uadilifu, tabia njema na muwape makuzi mema," alisema.



Waziri wa Tamisemi, Mohamed Mchengerwa.

# Serikali yashtuka usalama wa watoto Lindi

## ■ NGOs zashauriwa kuingilia kati

**Na Abdul Mitumba, Ruangwa**

SERIKALI Wilaya ya Ruangwa mkoani Lindi, imesema haina uhakika wa maisha ya watoto hasa wanafunzi wadogo wanaoachwa na wazazi wao kwa muda mrefu, kufuatia wazazi hao kukimbilia mashambani kwa ajili ya kilimo cha zao la ufuta.

Inasema, kitendo cha wazazi na walezi kuwaacha watoto wadogo kwa zaidi ya miezi mitatu bila uangalizi wa uhakika, ni ukatili na hatari kwa ustawi wa maisha yao hasa katika maendeleo ya elimu.

Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa, Hassan Ngoma, alielezea wasawasi huo mbele ya viongozi wa mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) ya wilayani humu na kuwataka kuandika miradi ya kusaidia jamii iangalie upya mfumo wa malezi ya watoto.

"Inashangaza kuona wazazi na walezi wanawaacha watoto mjini au vijijini peke yao na kwenda umbali mrefu mashambani kwa muda mrefu bila uangalizi madhubuti. Andikeni maandiko muombe fedha ili mje mtoe elimu kwenye eneo hili tusaidie jamii yetu kuona umuhimu wa kutunza familia bila kuathiri shughuli za kiuchumi ikiwemo kilimo," alisema Ngoma.

Aliongeza kuwa wakati wazazi na walezi wakiwa mbali na watoto, makundi ya watoto kuanzia wanne na kuendelea, hutembea kutoka eneo moja hadi kusikojulikana, hali inayoongeza shaka juu ya usalama wao.

"Katika mazingira kama haya, ni rahisi watoto kuhujumiwa na kufanyiwa matukio ya kikatili ikiwemo kubakwa na kulawitiwa. Kama viongozi wa asasi za kiraia, mnaowajibu wa kuliangalia eneo hili kwa macho ya ziada," alisema.

Akizungumzia ombi la Mkuu wa Wilaya, Ofisa Tathmini na Ufuatiliaji wa Asasi ya Kuunganisha Vijana Kimaendeleo Ruangwa (Akuvikiru), Bahati Mtapa, alisema mashirika yanashindwa kufanya baadhi ya miradi kutokana na wafadhili kutoa fedha huku wakielekeza aina ya miradi ya kutekeleza.

Katika kipindi cha Januari hadi Machi, kila mwaka, wakati wengi wa wilaya ya Ruangwa, huyaacha makazi yao na watoto mijini na vijijini kwenda mashamba ya mbali na makazi kulima mashamba ya ufuta, hivyo kuwaacha watoto wadogo na upweke.




Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa, Hassan Ngoma



# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi

## HII NI KERO

### Matunda 'feki' yadhibitiwe



Katika masoko kama ya Temeke Stereo, unaweza kununua papai, juu lina rangi nzuri lakini ukila halina ladha na mwisho unasikia uchungu. Kumbe ni mapapai 'yanayolazimishwa' kuiva kwa kutumia moto.

Hali ni hiyohiyo kwenye matunda mengine kama maembe, ndizi na kadhalika. Hii kwa kweli ni mbaya sana. Mamlaka husika zinapaswa kusimamia mazao yanayoingia kwenye masoko ili kudhibiti ubora. Wakulima kwa kulazimisha kuuza matunda machanga hamtendi haki. Mbona machinjioni kuna maofisa wanaodhibiti ubora wa nyama kwa nini isiwe hivyo kwenye masoko pia?




MAONI YA MHARIRI

# Tulinde vizuri vya kwetu

KATIKA kuadhimisha miaka 60 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, keshokutwa Januari 12, kumekuwa na uzinduzi wa miradi mbalimbali visiwani humo.

Tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kwa kupeleka fedha kwenye miradi hiyo lukuki inayolenga kubadilisha maisha ya Watanzania hao wanaoishi Unguja na Pemba.

Katika uzinduzi wa miradi hiyo, viongozi wetu wamekuwa wakitoa kauli mbalimbali muhimu za kufanyia kazi, kubwa ikiwa ni kulinda miradi hiyo idumu na ilete manufaa kwa wananchi.

Jana, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, alizindua Jengo la Kitega Uchumi la Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC).

Kama ilivyotazamiwa, alitoa maelekezo muhimu ya kufanyia kazi. Moja ya maagizo hayo ni kutaka hadhi, ubora na chapa ya karafuu inayozalishwa Zanzibar ilindwe.

Rais alisema karafuu visiwani humo ni sawa na madini ya almasi au dhahabu kwa kuingiza fedha nyingi za kigeni. Alitoa mfano wa mwaka 2022 ambapo karafuu iliingiza Sh. bilioni 118, sawa na asilimia 65.6 ya mauzo yote ya Zanzibar nje ya nchi.

Alisema zamani karafuu ilikuwa ikiuzwa kwa mtu mmoja au wawili ambao walikuwa wakichanganya na karafuu kutoka nchi zao ili kupata ladha ya karafuu ya Zanzibar na kwenda kuuza kwenye masoko ya dunia.

Lakini akasema kwa sasa karafuu ya Zanzibar, inakwenda yenyewe kwenye soko la kimataifa na ndiyo maana bei ya zao hilo imekuwa imara.

Alisema kwa kuzingatia upekee na umaarufu wa karafuu ya Zanzibar katika soko la kimataifa kila mmoja anapaswa kuhakikisha kwamba chapa ya karafuu ya Zanzibar na umaarufu wake unaendelea kubaki uleule.

Aliahidi kwamba serikali zote mbili, zitaendelea kutafuta masoko ya karafuu nje ya nchi na kwamba kazi itakua rahisi kama hadhi, ubora na chapa ya karafuu ya Zanzibar itabaki kama ilivyo wakati huu serikali inapotafuta njia za kisayansi kuongeza tija na uzalishaji wa zao hilo.

Tunawahimiza wahusika kufanyia kazi maagizo yote ya Rais Samia, likiwemo hilo la kulinda ladha ya karafuu, lakini ni vyema hilo likafanyika pia kwa mazao yote yanayozalishwa nchini mwetu.

Kumekuwepo na habari za majirani zetu ambao wamekuwa wakichukua mazao ya Tanzania, kama maparachichi, unga wa mahindi, maziwa ya ng'ombe na kadhalika, wakayachakata, wakaweka nembo zao za ubora na msimbo mpau (barcode) kwamba yanazalishwa katika nchi hiyo ya jirani.

Zipo pia taarifa za maziwa ya Tanzania yanayotokana na ng'ombe wetu wa kienyeji na hata mahindi, kununuliwa Tanzania na majirani kuyaweka kwenye mifuko kisasa na kuuza kwa kutumia nembo zao. Iliwahi kudhaniwa pia kwamba Tanzanite inatoka nchi jirani na wengine kudhani inatoka India!

Ni vyema wasaidizi wa Rais waendelee kuhakikisha tunalinda vitu vyetu na kuviuza nje vikiwa na nembo ya Tanzania. Hebu fikiria kusikia kwamba wapo Watanzania walipokwenda nje na maparachichi, iliwachukua muda kuwathibitishia wanunuzi kujua kwamba hata maparachichi wanayodai yanatoka kwa majirani zetu, kimsingi yanatoka Tanzania!

Kama wenzetu wanaweza kuwa makini (aggressive) kwenye soko hadi kuuza vya kwetu wakidai ni vyao, na sisi hatuna budi kuamka na kuhakikisha tunalinda vizuri vya kwetu kuanzia vyakula, viungo hadi madini.


## Wasiliana nasi

**Mhariri Mkuu:** +255713263775 / +255748115000
**Mhariri wa Habari:** +255768411003
**Mhariri Michezo:** +255787559090
**Meneja Masoko/Biashara:** + 255718480406 / + 255733768825
**S. L. P:** 15110, Dar es Salaam
**Makao Makuu Mtaa:** Barabara ya Morogoro
**Jengo la:** Aura Mall
**Chumba Cha Habari:** +255 (0)222151532
**Email:** uelekeohabari@gmail.com


Na Abdul Mitumba, Ruangwa

## JICHO LANGU

# TGNP: Wanahabari zingatieni haya kipindi cha uchaguzi

MWAKA huu wa 2024, Tanzania inatarajiwa kuwa na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji, kabla ya Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani kufanyika mwakani.

Ni kipindi adhimu kwani ndicho kitakachotupa wawakilishi wetu katika kipindi kingine cha miaka mitano. Moja ya wadau muhimu katika kuwafikishi wananchi habari, ni waandishi wa habri.

Kwa kujua umuhimu wao, Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), imeviomba vyombo vya habari vya ndani kujiandaa kikamilifu ili kuripoti kwa haki matukio yanayohusu haki za wanawake katika kugombea, kuchagua na kuchaguliwa nafasi mbalimbali za uongozi katika changuzi mbili kubwa zijazo.

Ikumbukwe kwamba, wakati vyama vya siasa hutoa ilani zao za uchaguzi, hata taasisi mbalimbali zinaweza pia kutoa ilani zao nja hata wanahabari!

Kwa mujibu wa Ilani ya Uchaguzi ya Wanawake kwenye chaguzi hizo iliyotolewa na TGNP ikishirikiana na Mtandao wa Wanawake na Katiba na Mfuko wa Wanawake Tanzania (WFT), inaamini vyombo vya habari vikitenda haki katika kuripoti matukio, nchi itabaki salama wakati wa kampeni, kupiga kura na baada ya matokeo kutangazwa.

Wakati wote wa uchaguzi, vyombo vya habari ni mhimili mkuu unaounganisha wagombea na wapiga kura, pamoja na kutoa viashiria vinavyoweza kusababisha vurugu na machafuko," imesema sehemu muhimu ya Ilani hiyo TGNP na washirika wake yenye kusara 39.

Ilani inasema ni vyombo vya habari vina uwezo wa kutoa fursa na jukwaa la kujadili masuala yeti yanayohusu mustakabali wa taifa kwenye maeneo mengi ikiwemo ya jinsia. Pia TGNP na washirika wake wanasema vyombo vya habari vina nguvu kubwa ya kuwezesha mabadiliko ya mfumo kandamizi kwa kukemea ubaguzi wa aina yoyote, vitendo vya rushwa hasa ya ngono kwa wagombea wanawake wakati wa uchaguzi.

Katika Ilani hiyo, TGNP imeainisha maeneo 13 ya msingi na muhimu yanayopaswa kuzingatiwa na vyombo vya habari wakati wa uchaguzi, kuanzia kuandikisha wapiga kura, kampeni na kutangazwa matokeo.

> **Wakati wote wa uchaguzi, vyombo vya habari ni mhimili mkuu unaounganisha wagombea na wapiga kura, pamoja na kutoa viashiria vinavyoweza kusababisha vurugu na machafuko," imesema sehemu muhimu ya Ilani hiyo TGNP na washirika wake yenye kusara 39.**

Moja, vyombo vya habari vinavyomilikiwa na umma, vihakikishe vinakuwa na mpango madhubuti unaotoa taarifa ya kuelimisha umma wa Tanzania kuhusu haki za wanawake katika kushiriki kwenye chaguzi zote.

Mbili, vyombo vya habari vikiwemo vya mtandaoni vikemee na kujiepusha na tabia za ukatili dhidi ya wanawake.

Tatu, Baraza la Habari Tanzania (MCT) pamoja na vyombo vyote vinavyosimamia utoaji wa habari, vihakikishe kunakuwa na mifumo ya uwajibikaji katika kutoa taarifa ili kudhibiti habari za kuwadhalilisha wanawake wagombea na wapiga kura.

Nne, vyombo vya habari vyenye kudai uhuru wa kutoa na kupokea habari, vijihusishe zaidi na kuandika makala mbalimbali na kutayarisha vipindi maalumu vinavyolenga kuibua mjadala wa kitaifa kuhusu ushiriki wa wanawake katika uchaguzi na faida zake.

Tano, vyombo vya habari viwape wagombea wanawake kipaumbele kwenye matamko yao wakati wa kampeni. Pia wanahabari watoe taarifa kuhusu vitendo vinavyosababisha ushiriki mdogo wa wanawake katika uchaguzi.

*Itaendelea.*

## VITA VYA ISRAEL, HAMAS:

# Silaha mpya za teknolojia ya juu za Israel huko Gaza





**Na Mwandishi Wetu**

VIKOSI vya Jeshi la Israel (IDF), ni mojawapo ya majeshi yenye uwezo mkubwa duniani.

Vita vya Gaza vimeshuhudia matumizi ya silaha mpya za teknolojia ya hali juu zilizoundwa na Israel.

Ujasusi wa kutumia akili mnembe au bandia, unachukua sehemu kubwa katika silaha za Israel na utambuzi wa shabaha ingawa uamuzi wa kuua unabaki kwa askari, kulingana na IDF.

Idadi ya waliofariki dunia Gaza imepita watu 22,000 kwa mujibu wa Wizara ya Afya ya Ukanda wa Gaza, inayoendeshwa na Hamas.

IDF inasema inafuata sheria za kimataifa na inachukua tahadhari ili kupunguza majeruhi kwa raia.

Silaha mpya zinazotumiwa na Israel

- Afisa wa jeshi la Israel akiri 'uharibifu mkubwa' katika kambi ya wakimbizi Gaza
- Vifaru vya Barak

Vifaru vya Barak, vinaelezewa kuwa ni toleo la tano la vifaru vya Merkava. Vinatumia akili bandia. Vinamwezesha kamanda aliyeko ndani, kuona nje hata kama funiko la juu limefungwa.

Vifaru hivi vipya viliwasilishwa kwa vikosi vya Israel Septemba, mwaka jana baada ya miaka mitano ya kutengenezwa.

Barak pia ina mfumo wa kujilinda. Huunda kinga ya digrii 360 kuzunguka kifaru. Mfumo huo hutambua mara moja tishio lolote na hurusha kombora na hulipua kombora linalokuja.

### Droni za Spark

Droni za Spark zimeundwa kama sehemu ya mpango wa Jeshi la Anga la Israel. Zimeundwa na kampuni za Rafael Advanced Defence Systems na Aeronautics Group.

IDF haijafichua mengi kuhusu ndege hizi mpya. Imesema zitaboresha kwa kiasi kikubwa ufanisi na uwezo wa askari wanaoendesha mashambulizi, kulingana na taarifa wanazopokea kutoka katika droni hizo.

Lakini IDF haielezi droni hizo zinafanyaje kazi.

### Droni ya kilo tatu

Hizi ni katika toleo la ndege zisizo na rubani za Kamikaz, zina uzani wa kilo tatu tu na uwezo wa kubeba kombora moja.

Kulingana na mtengenezaji, hutumiwa zaidi katika maeneo askari wasiyoweza kuona. Inamaanisha zinaweza kuruka katika maeneo ya adui ambayo askari anayefanya kazi chini hawezi kuona.

Ndege hiyo isiyo na rubani, ina uwezo wa kubaki hewani kwa hadi dakika 30 na kuwapa wanajeshi ufahamu wa hali ya mambo hadi kilomita 1.5.



Inakusanya taarifa na kuonyesha shabaha kwa amri ya askari ambaye anaidhibiti kwa kompyuta. Inaweza kurudi kambini au ikiwa na kichwa cha kombora inaweza kushambulia shabaha.

### Kombora la Iron Sting

Hutumia mionzi na GPS limeundwa na kampuni ya ulinzi ya Elbit. Limetumika kwa mara ya kwanza Gaza Oktoba, mwaka jana kwa mujibu wa IDF.

Kama ilivyoelezwa na mtengenezaji, Iron sting lina urefu wa milimita 120 ni kombora linaloongozwa na hushambulia shabaha kwa usahihi. Linaweza kushambulia shabaha ya umbali wa kilomita 1-12.

Kombora hilo linaweza kupenya kuta nene za zege na kulipua, kulingana na Elbit.

### Akili bandia katika vita (AI)

Matumizi ya akili bandia katika vita yanaelezwa huifanya silaha kushambulia kwa usahihi zaidi na hivyo kupunguza uharibifu usiohitajika na mauaji ya wasio na hatia.

Umoja wa Mataifa na Kamati ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu (ICRC), wameelezea wasiwasi wao kuhusu matumizi ya akili bandia.

ICRC imesema katika ripoti iliyotolewa mapema mwaka jana, wajibu wa kisheria na wajibu wa kimaadili katika vita hayapaswi kutolewa na mashine na programu.

Wasiwasi huu unahusiana na mifumo ya silaha zinazojiendesha; mifumo ambayo mara inapoachiliwa hufanya kazi kwa uhuru kulingana na programu zake.

Mwaka jana, IDF imetumia akili bandia kukusanya taarifa za kijasusi na kushambulia shabaha. Mifumo ya akili bandia ilikuwa inatumiwa tayari na Israel katika vita vya siku 11 huko Gaza mwaka 2021.

Katika mahojiano na tovuti ya habari ya Israel ya Ynet News Juni, mwaka jana, Mkuu wa zamani wa Vikosi vya Ulinzi vya Israel, Aviv Kochavi, alitaja kitengo cha Targeting Directorate kinajumuisha mamia ya maafisa na wanajeshi, wanaofanya kazi kwa kutumia mfumo wa akili bandia.

"Ni mifumo ambayo huchakata kiasi kikubwa cha data haraka na kwa ufanisi zaidi kuliko binadamu yeyote na kuzitafsiri katika malengo yanayotekelezeka," alisema na kuongeza:

"Katika siku za nyuma, tungegundua shabaha 50 huko Gaza kwa mwaka mmoja. Sasa mifumo hii huonyesha shabaha 100 kwa siku moja."

### Mfumo wa Gospel

Mfumo wa Gospel umeundwa nchini Israel kwa kutumia akili bandia unaendeshwa na Targeting Directorate na unafanya kazi saa 24, kama ilivyoelezwa na IDF katika makala iliyochapishwa kwenye tovuti yao Novemba 2, mwaka jana.

Mfumo huu huonyesha shabaha kwa kuchakata kiasi kikubwa cha data zilizokusanywa na mashirika ya kijasusi ya Israel katika Ukanda wa Gaza.

Hata hivyo, uamuzi wa utekelezaji unasalia mikononi mwa maafisa, kulingana na IDF.

Siku ya 27 ya vita, IDF ilisema kulikuwa na shabaha zaidi ya 12,000 katika Ukanda wa Gaza.

Yuval Abraham, Mwandishi wa Habari wa Uchunguzi wa Israel anayeishi Jerusalem, amekuwa akichunguza matumizi ya akili bandia katika vita vya Gaza.

Ripoti ya Abraham "Mass assassination factory" iliyoandikwa katika gazeti la +972 - gazeti huru la mtandaoni la waandishi wa habari wa Palestina na Israel.

Ripoti hiyo inatokana na mazungumzo na maafisa saba wa sasa na wa zamani wa mashirika ya kijasusi ya Israel, wakiwemo maafisa wa kijasusi wa kijeshi na wanajeshi wa anga ambao walihusika katika operesheni za Israel.

Abraham aliiambia BBC, mfumo wa Gospel hutoa taarifa kuhusu wanaotaka kushambuliwa na nyumba zao pamoja na idadi ya raia ambao IDF huenda ikawaua.

IDF iliiambia BBC kuhusu madai hayo: "Katika kukabiliana na mashambulizi ya kikatili ya Hamas, IDF inafanya kazi ya kuharibu uwezo wa kijeshi na kiutawala wa Hamas. IDF inafuata sheria za kimataifa na huchukua tahadhari zinazowezekana ili kupunguza madhara ya raia."



### Mabomu yanayoongozwa na yasiyoongozwa

Tathmini ya Ofisi ya Mkurugenzi wa Ujasusi wa Kitaifa wa Marekani iliyotolewa Desemba, mwaka jana, ikafichuliwa na CNN inasema, karibu asilimia 40 hadi 45 ya mabomu 29,000 ambayo Israel iliangusha Gaza, hayakuwa mabomu ya kuongozwa.

"Mabomu yasioongozwa yanaweza kukosa shabaha kwa hadi mita 30," Marc Garlasco, mchambuzi wa zamani wa kijasusi wa Pentagon na mchunguzi wa zamani wa uhalifu wa kivita wa Umoja wa Mataifa, aliiambia BBC.

**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, wakati akifungua Jengo la Kitega Uchumi la Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC), Pemba, Zanzibar.**














Jarida hili haliuzwi

*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

Uelekeo

JARIDA

# Jungu Jkuu

| Jumatano Januari 10 - 16, 2024 |

KOLAMU JAMII SIASA



# Dk. Mwinyi na kimbunga cha maendeleo Zanzibar

UK. 12 & 13

Mazingira



# Tubadilike, tulinde mazingira ipasavyo

**Na Dk Felician Kilahama**

NAMSHUKURU Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia zawadi ya uhai na afya njema hadi wakati huu tunapotafakali kuhusu uharibifu wa mazingira Tanzania. Hii ni Sehemu ya tatu ya makala inayoangalia mvua za El-Nino na madhara yake kwa Watanzania, mijini na vijijini kutokana na mafuriko hatarishi yasiyotegemewa.

Katika sehemu ya Pili tulihitimisha kwa kuainisha kuwa kupitia kilimo kisichokuwa endelevu (kufyeka misitu, kuchoma moto na kuchunga mifugo kiholela); kumesababisha changamoto za uharibifu wa ardhi kutokana na maeneo mengi kuwa wazi bila uoto wa asili.

Hali hiyo huchochea mmomonyoko wa udongo kupitia kasi ya maji ya mvua pamoja na nguvu ya upepo mkali. Maji na upepo husomba au kupeperusha chembechembe za udongo na kuzipeleka mabondeni hadi kwenye mito, mabwawa na katika maziwa.

Kwa miongo takribani minne, kina cha Mto Msimbazi (river bed) ambao tunaufanyia rejea zaidi kuwakilisha mito mingine, kilikuwa chini, kirefu katika mazingira asilia. Vilevile, hali ya mazingira kwenye eneo la kandokando ya mto huo yalikuwa ya kuridhisha sana; maji yalikuwa yanapita na kutiririka bila kukumbana na takangumu wala udongo au mchanga.

Maji yanapotiririka kwenye mto kutoka ukanda wa juu na kuelekea ukanda wa chini; kasi yake hupungua kadri mto unavyokaribia bahari. Haliha lisi ni kwamba sehemu kubwa za udongo, mchanga na takangumu hutua/kugota chini taratibu wakati mkondo wa mto unapokuwa unaingia baharini au ziwani.

Kadri miaka inavyozidi kupita kina cha Mto Msimbazi na mito ningineyo nchini, huendelea kupungua na kuathiri sana usafirishaji maji nyakati za mvua za vuli na masika. Matokeo yake ni mafuriko kutokana na vina vya mito kujaa ama udongo, mchanga au takangumu.

Uzoefu umeonesha kuwa takribani miongo mitatu iliyopita, kuanzia miaka ya 1980 hadi sasa shughuli za kibinadamu ambazo siyo rafiki kwa mazingira, zimekuwa zikiongezeka sana. Miaka hiyo ya nyuma, maji ya mvua yalikuwa yakitiririka kutoka mwanzo wa mto hadi mwisho bila kuzidi kwenye kingo za mto wala kujaa udongo/mchanga na takangumu.

Ni mara chache maji yaliweza kuvuka kingo za mito kutokana na mvua nyingi kupita hali ya kawaida.

Pamoja na hayo, hapakuwepo mikakati madhubuti ya kulinda mazingira karibu na mito. Kwa mfano, wataalamu wa mazingira hawapo vijijini na pia mijini bado ni wachache sana. Udhaifu huo ukiunganishwa na wanasiasa kuwa na mitazamo tofauti kuhusu kuhifadhi mazingira, hali kwenye mazingira ya mito ikaendelea kuzorota takribani kila sehemuu.

Kadhalika, vijiji vikawa havina mipango endelevu ya matumizi bora ya ardhi ndani ya mipaka ya vijiji na vitongoji husika. Athari sasa zimekuwa kubwa sana mathalani, tunapopita eneo la Mto Msimbazi; (barabara ya Morogoro) tunaona machine aina ya 'caterpillars' zikikazana kuondoa udongo na takangumu mtoni; hivyo kutengeneza vilima kando ya mto.

Ukitafakari kwa undani zaidi, utagundua kuwa miongoni mwetu wamekosa maarifa au kwa dhamira binafsi wakavaa 'roho' za kutojali usitawi wa mazingira.

Tunapokumbwa na mafuriko na kupoteza mali na wakati mwingine baadhi ya wananchi kupoteza maisha; au ukame ukizidi hadi kusababisha njaa kali, tunalalamikia mabadiliko ya tabianchi kumbe mabadiliko hayo ni binadamu wenyewe tumeyasababisha kwa kufanya shughuli mbalimbali zisizorafiki wa mazingira.

Mthalani, mataifa tajiri kuendelea kuzalisha gesiukaa kwa wingi kiasi cha kuathiri hali ya ukanda wa ozoni angani na kupelekea ongezeko kubwa la joto duniani.

Wakati huohuo, nchi zinazoinukia kiuchumi kama Tanzania zinakazania pia kuinua hali ya maisha ya kila siku na katika harakati hizo uharibifu wa mazingira unazidi kuongezeka kiasi kwamba matokeo yake ni 'majuto' na 'mahangaiko makubwa' kwa Watanzania wengi vijijini na mijini.

Kinachojiri kwenye Mto Msimbazi, Jijini Dar es Salaam na sehemu nyingine nchini ikiwemo yaliyojiri Hanang hivi karibuni ni kielelezo kwamba tulijisahau na kufanya mambo kinyume na matarajio chanya.

Ile lugha ambayo nilikuwa naisikia kutoka kwa baadhi ya viongozi wakisema "waache wananchi msiwabughudhi, wanaganga njaa"; wengi wetu sasa ndio tunaganga njaa.

Iwapo tungezingatia misingi ya kutunza mito hali isingekuwa kama ilivyo sasa. Serikali isingelazimika kutumia gharama kubwa aidha kujenga daraja la juu kutoka Magomenu Mapipa mpaka eneo la Faya wala kulazimika kuwahamisha watu waliojenga hadi kingo za Mto Msimbazi.

Maeneo yaliyoonekana kuwa muhimu enzi za wakoloni na yakahifadhiwa: wakati huo idadi ya watanzania na mifugo ilikuwa siyokubwa. Pamoja na uchache huo; wakaoloni waliona upoulazima wa kuyahifadhi Kisheria.

Baada ya kujitawala, baadhi yetu tukaanza kuona kuwa hakuna sababu ya msingi kuendelea kuyahifadhi. Watanzania tujiulize maeneo husika ambayo wakoloni waliyahifadhi kati ya 1930 na 1960 je, walifanya hivyo bila sababu za msingi?

Kwa ujumla, mengi ya maeneo yaliyohifadhiwa ni muhimu sana kwa mustakabali mzima wa taifa na Watanzania kwa ujumla. Kwanza, yamesheheni uotoasili unaosaidia sana kuhifadhi vyanzo vya maji (misitulindimaji). Kadhalika, kwenye maeneo hayo kuna baioanuai (mimea na wanyama) zenye umuhimu mkubwa kimataifa (biodiversity) kiasi kwamba baadhi ya mimea na wanyama hupatikana kwenye maeneo hayo hapa Tanzania tu na siyo kwingineko duniani.

Pili, ni maeneo yenye umuhimu wa pekee wa kuhifadhi ardhi na uotoasilia ili kuzuia mmomonyoko wa udongo hivyo kuepuka makorongo makubwa kama hali ilivyokuwa eneo la Haubi, Wilayani Kondoa; baada ya kupata uhuru wa Tanganyika mwishoni mwa 1961.

Kuna usemi usemao "yaliyopita si ndwele, tugange yajayo"; sasa Tanzania tupo njiapanda, mazingira sehemu mbalimbali vijijini na mijini yamejeruhiwa kwa kiasi kikubwa. Katika maeneo yaliyohifadhiwa Kisheria nako huko hali sishwari.

Hifadhi kadhaa za misitu hasa misitu ya uzalishaji mazo-misitu yanayotakiwa kwa maendeleo ya taifa; zimegeuzwa 'mashamba ya bibi' ambako kila mtu anafanya anavyotaka; maana usimamizi wake umelegalega sana.

Hali hii inatia moyo wenye misitulindimaji au yenye umuhimu mkubwa kimataifa angalau huko usimamizi umeimarishwa.

Watanzania wote mijini na vijijini, tujitathmini ipasavyo, tulipotoka na tunakokwenda kwa kuangalia nini visababishi husika na tujue njia sahihi ya kuondoa vikwazo ili mazingira kwa ujumla wake yasiendelee kuharibika na kusababisha madhara makubwa nchini mathalani, mafuriko kutokana na El-Nino yaliyopiga sehemu mbalimbali za nchi yetu Novemba, 2023 hususani Hanang.

Vilevile, tujiulize nini kifanyike? Wataalamu waongezewe nguvu hasa wanapokazana kuhakikisha mazingira, yanatunzwa kwa faida ya wote.

Mipango yote kuanzia vijijini hadi taifa; mipango ya maendeleo (muda mfupi na mrefu) izingatie umuhimu wa kutunza na kuendeleza mazingira. Shughuli za binadamu zisipelekee kuharibu vyanzo asilia vya maji; misitu ya asili na mapori vilindwe hasakwa iliyohifadhiwa kisheria.

Vijiji vitenge maeneo yenye hali bora ya misitu na kuyahifadhi kisheria hususani kupitia mipango ya vijiji kwa matumizi bora ya ardhi; kwa kuzingatia Sheria ya Ardhi vijijini na Kanuni zake na Sheria ya Misitu (CAP323:RE 202).

Shughuli za ugani na elimu ya mazingira kwa wananchi ziimarishwe na wataalamu wawezeshwe ipasavyo ili huduma za ugani, ufuatiliaji na uperembaji zifanyike ipasavyo.

Vilevile, kuwepo na ushirikiano kitaaluma mfano, kilimo, mifugo, umwagiliaji, misitu, ufugaji nyuki, wanyamapori, uvuvi, maendeleo ya jamii, biashara na viwanda na wengineo.

Wataalamu wa fani za uhasibu, mipango, ukaguzi na manunuzi/ugavi; ni maeneo mtambuka hivyo wanafiti kwenye makundi mbalimbali ya kitaaluma. Nia iwe ni kujenga mshikamano katika kuiwezesha Serikali kufanya maamuzi sahihi (well-informed decisions); kwa kujikita zaidi kwenye misingi ya kitaaluma.

Naamini kukiwepo mshikamano wa hali ya juu kati ya viongozi, wataalamu na wananchi kwa ujumla; taifa litapiga hatua kubwa katika kujiletea maendeleo endelevu. Roho za ubinafsi na kutowajibika ipasavyo hazitapata nafasi.

Lengo kuu likiwa kuimashisha na kuendeleza Maisha bora kwa Watanzania wote pamoja na kuhakikisha kuna usalama wa chakula na lishe, umoja wa kitaifa na amani. Hivyo, tunatakiwa kuimarisha amani na usalama wa kutosha kwa kila Mtanzania na mali zake.

Yote hayo yanawezekana iwapo kila mwenye nguvu atafanyakazi kwa bidii na maarifa na kutimiza wajibu ipasavyo. Nathubutu kusema: "Tanzania bila umaskini wala njaa inawezekana"; kinachotakiwa ni kila mwenye nguvu afanye kazi kwa bidii kwa manufaa yake, familia na taifa kwa ujumla.

Vilevile, tunapofanyakazi tutumie akili na maarifa ili kuhakikisha kunakuwa na matumizi bora ya ardhi na vyote vilivyopo chini au juu yake. Vilevile, kazi za mikono yetu ziwe 'rafiki wa mazingira' kwa mustakabali mzima wa maisha ya vizazi vijavyo.

Watanzania tumerithi nchi yenye rutuba na maliasili tele kutoka kwa mababu sasa tubadilike tuhakikishe mazingira yanatunzwa nyakati zate.

Tuwe wenye 'busara kama nyoka' zaidi ya hapo tuwe na 'maarifa ya kimbingu' kiasi kwamba 'tuzijenge nyumba zetu kwenye miamba' ambako hata yakitokea mfuriko au dhoruba kali bado tutakuwa salama.

Lakini tukiendelea kujenga nyumba katika ardhioevu au michanga basi tujue dhuruba na mafuriko hayatuachi na hivyo tutaendelea kuwa na mahangaiko yasiyokuwa na mwisho.

Hakuna lisilowezekana, tuchukue hatua na kufanya uamuzi sahihi kwa weledi mkubwa, hekima na maarifa kwa faida ya sasa na vizazi vijavyo.

Mungu ibariki Tanzania na watu wake.



Hamisi Kibari

TUKUBALIANE KUTOKUBALIANA

Simu: 0758143457

# Imani za kishirikina bado tatizo

"UNAJUA hapa wanasema nini kuhusu kilichomuua marehemu?" Aliniuliza mmoja wa ndugu zangu tukiwa tumeketi msibani tukisubiri chakula cha usiku.

"Mbona kilichomuua kinajulikana!" Nikamjibu.

"Si huo ugonjwa unaodhani. Habari zimeenea hapa kwamba nanihii (akamtaja jina) ndiye amemuua kwa chuki tu za kijinga. Kwani hujasikia?"

"Sijasikia, lakini kama kuna wanaoamini hivyo, si kweli," nilijibu. Yule jamaa yangu akanisogelea zaidi ili kunipa 'mchapo'.

"Sikiliza. Usidhani kwamba uchawi haupo. Tatizo mkisoma na kuishi mjini mnadharau haya mambo. Uchawi upo!" Akasema.

"Hata mimi ninajua uchawi upo kwa sababu umetajwa pia kwenye vitabu vitakatifu. Sisi Waislamu tunajifunza kwamba Mwenyezi Mungu aliumba uchawi kama sehemu ya mitihani, lakini marehemu ninajua kilichomuua na hata wewe unajua."

Akanyamaza kidogo kisha akanigeukia. "Sikiliza wewe unayejifanya mtu wa dini. Inaelezwa kwamba huyu bwana (akamtaja tena jina) uchawi aliutoa kisiwani, akamwekea marehemu kwenye chakula."

Nikalazimika kumfafanulia huyo ndugu yangu katika ukoo kwamba marehemu ambaye tulikuwa tumemzika jioni hiyo (Mwenyezi Mungu amrehemu) mimi nilishiriki katika matibabu yake alipokuwa amelezwa katika Hospitali maalumu ya magonjwa ya saratani pale Ocean Road, Dar es Salaam.

Ni mgonjwa ambaye madaktari siku wanampokea na kisha vipimo kadhaa kuchukuliwa walionesha dhahiri kwamba saratani ya koo ilikuwa imeshamla sana marehemu na kulaumu kwa nini amecheleweshwa kiasi kile.

Nikamwambia ndugu yangu huyo kwamba kama anataka kushika mtu uchawi katika hilo basi ni heri awashike madaktari wa hospitali za awali, hususani pale Musoma, ambao walichelewa kugundua tatizo ama kumpa rufaa baada ya kuona hali ya mgonjwa inazidi kuwa mbaya.

Nikasema licha ya madaktari pale Ocean Road kujitahidi sana kumpiga mionzi baada ya operesheni, hali ilikuwa imeshakuwa mbaya na hivyo hawakuweza kuokoa maisha yake. Nikasema huyu ni mgonjwa kati ya wengi wanaougua saratani hapa nchini mwetu, ugonjwa ambao unaua watu wengi sana pengine kuliko hata ajali na nikamtaka ndugu huyo siku moja akipata nafasi ya kufika Dar es Salaam, afike pia pale Ocean Road kama anataka kujua ukubwa wa tatizo!

Nikafafanua kwamba ugonjwa huu wa saratani ambao, kama ilivyo kwa magonjwa ya kisukari ama shinikizo la damu, madaktari wanatuambia kwamba baadhi ya sababu zake ni vyakula vya siku hizi tunavyokula baadhi vikiwa vimeisha muda wake ama kemikali wanazotunzia, kuvuta sigara na kutofanya mazoezi.

Nikamwambia kwamba ingawa saratani nyingine hazifahamiki chanzo chake, lakini hata baadhi ya dawa bandia au zilizoisha muda wake tunazonunua kwenye maduka ya dawa zaweza kuwa chanzo cha saratani!

Nikazidi kumsisitizia ndugu yangu yule kwamba badala ya kulaumu ama kupambana na mtindo wa siku hizi wa maisha unaochangia magonjwa haya ama hata kulaumu madaktari waliochelewa kugundua kwamba marehemu alikuwa anasumbuliwa na saratani, wao wanashika uchawi mtu ambaye nina hakika kwa asilimia 100 hahusiki na 'kumroga' ndugu yetu katika ukoo tuliokuwa tumemzika jioni hiyo.

Kwamba mtuhumiwa huyo anaweza kuchukiwa ama hata kuchomewa nyumba kutokana na tuhuma ambazo hahusiki nazo abadani.

Pamoja na kusema sana hadi midomo ikanikauka lakini ilikuwa kama ninampigia mbuzi gitaa. Bado sikufanikiwa kumwondosha ndugu yangu huyo katika imani za 'ulozi' na nilipozidi kusema akaniita mbishi, nisiyejua mambo na mtu ambaye maisha ya mjini yamenipumbaza!

Nakumbuka si marehemu huyo pekee ambaye kifo chake kilihusishwa na kurogwa bali ninawajua wengine pia. Kwa takribani misiba minne niliyoitembelea pale Musoma kwa ajili ya kuhani kwani ilitokea nikiwa Dar kwenye 'utafutaji' hakuna ambao marehemu wake alikufa kifo cha kawaida isipokuwa kurogwa!

Kwa mfano, upo wa huyu ndugu yangu mwingine aliyekuwa askari polisi, naye niliambiwa aliugua na hatimaye kufa baada ya kula chakula kwa ndugu yetu mmoja aliyemtilia uchawi.

Msiba mwingine ulikuwa wa mtoto wa shangazi yangu, ambaye hakuna asiyejua kwamba alikufa kutokana na kuacha kutumia dawa za kufubaza virusi vinavyosababisha ugonjwa wa ukimwi (VVU) na hivyo tatizo lake likawa kubwa.

Kwa muda mrefu, huyu alishapima na kugundulika tatizo lake lakini baadaye akaacha tiba sahihi na kugeukia waganga akidanganywa kwamba 'kalogezewa' ukimwi (sijui kama 'kulogezewa' ni Kiswahili au Kijita!). Alipofariki dunia watu wakamwandama mtu waliyempachika kwamba ndiye mchawi wake kutokana na ramli chonganishi!

Lakini kilichonifanya kuandika makala haya ni mambo mawili, lile tukio la Geita la mwanamke anayedaiwa kufa na kuibuka akiwa hai na kilichompata kijana wangu aliyekuwa akinisaidia kazi nyumbani.

Baraka, kijana wa miaka 22 tu alianza kudai kujisikia uchovu mwingi na mwili kumuuma. Kuna hii siku alishindwa kabisa kufanya kazi zake, akaenda hospitali. Alipopima akagundulika kwamba alikuwa na kisukari na siku hiyo sukari ilifikia 20 (wenye ujuzi na ugonjwa huo wanajua maana ya 20).

Baraka, kijana mpole, mtu wa watu asiye na makuu, akaanzishiwa tiba na kupewa masharti. Ilishangaza kidogo kuona kijana mdogo kiasi hicho ana kisukari ambao ni moja ya magonjwa hatari (Mungu atuepushe ambao hatujaupata).

Siku tatu baadaye akazidiwa. Tukampeleka Hospitali ya Rufaa ya Temeke. Akawekwa kitengo cha dharura (Emergence) ambapo alipumzishwa kwa zaidi ya saa tatu na kuruhusiwa kurudi nyumbani baada ya sukari kushuka.

Siku chache baadaye akazidiwa tena. Tukampeleka hospitali, akalazwa kwa siku mbili. Alipotoka tukatakiwa tumwanzishie kliniki ya watu wenye kisukari.

Wakati hayo yakiendelea ndugu zake pale Magu wakawa wanashangaa na kumdai mtoto wao. Wakati 'tunajitafuta' ili aanze kliniki, sukari ikapanda tena. Safari hii akalazwa kwa siku nne mfululizo.

Alipotoka wodini, sasa alikuwa imara kidogo. Kwa vile ndugu zake walikuwa wakimdai, tukamsafirisha kurudi Magu ambako tuliamini pengine wanajua tiba bora zaidi. Ndiyo, zipo tiba za jadi zinazosaidia wengi.

Siku chache baada ya kufika Magu, sukari ikapanda tena. Baraka kalazwa. Akatibiwa na kupata nafuu. Badala ya kumwanzisha kliniki kama ulivyokuwa mpango wetu, wao wakampeleka kwa waganga wa jadi. Wakaamini Baraka alirogwa hapa Dar na watu waliomtoa Magu kabla hajaja kwangu.

Mganga tapeli akawaambia 'kalogezewa' kisukari na kwamba hilo ni dogo kwake. Baraka akazidiwa hadi akakata kauli. Waliposhtuka na kujaribu kumkimbiza hospitali, hakuwa Baraka tena, walikuwa wameshachelewa. Hivi tunavyoongea Baraka hatunaye duniani. Roho inaniuma sana kumpoteza huyu kijana kwa kuamini ushirikina. Kila nikimfikiria najikuta macho yakijaa machozi!

Kuna sakata la mwanamke wa Geita kudaiwa kufa, na kisha watu wakamwona akiwa hai. Madai ni kwamba alichukuliwa msukule na kuna mganga atajitokeza kwamba ndiye kamsalimisha kama sikosei. Sitalizungumzia kwa kina tukio hili kwa sababu bado ninalifuatilia lakini ninaamini ni imani nyingine za kishirikiana na michezo ya waganga wa jadi ili kutapeli wananchi!

Hata kama mkuu wa Wilaya hiyo amehusishwa lakini mimi haliniingii akilini abadan. Idadi ile ya watu nilioona kwenye klipu ya video wakimshangaa huyo mwanamama ndivyo imani za ushirikina zilivyo bado kwa watu wetu! Ni shida.

Kimsingi, neno 'ushirikina' maana yake halisi ni kumshirikisha Mwenyezi Mungu na viumbe vyake kwa maana ya kuabudu asiye Mwenyezi Mungu, kuomba asiye Mwenyezi Mungu (kama vile kuomba wafu) au kutegemea asiye mwenyezi Mungu (kama vile kutegemea hirizi ulioshonea kwenye nguo eti ndio mlinzi wako).

Hata hivyo, neno hili limeelekezwa zaidi kwenye watu wanaoamini waganga, uchawi, kupiga ramli na ujinga mwingine wa aina hiyo. Hata kwenye andiko hili, neno ushirikina limetumika kumaanisha hivyo.

Imani hizi potofu katika karne hii, baadhi zikisemwa na watu wanaoishi mijini na wakiwa na elimu ya viwango mbalimbali, zimekuwa zikinifanya nifikirie mengi sana. Kubwa ni jinsi jamii yetu inavyoendelea kuzama katika giza la imani hizi potofu licha ya maendeleo makubwa ya sayansi na teknolojia ambayo dunia imefikia leo kwa kuja na midude kama 3D na akili bandia (AI).

Nikakumbuka pia jinsi ambavyo bado ninaona mabango mbalimbali ya waganga wa jadi sehemu kama Dar es Salaama yakisomeka kwamba wana dawa za kusafisha nyota, dawa za akili kwa wanafunzi, dawa za kupata kazi ama kuvuta mpenzi au dawa za kunenepesha nyeti za wanaume!

Swali ambalo ninakuachia msomaji wangu ni hili. Nini kifanyike ili kuiokoa jamii yetu na imani hizi potofu? Pengine tunapopambana na mila potofu kama ukeketaji, tusisahau tatizo la imani za ushirikina. Bado zimekita mizizi!

**Hata mimi ninajua uchawi upo kwa sababu umetajwa pia kwenye vitabu vitakatifu. Sisi Waislamu tunajifunza kwamba Mwenyezi Mungu aliumba uchawi kama sehemu ya mitihani, lakini marehemu ninajua kilichomuua na hata wewe unajua.**

Maendeleo

# Dk. Mwinyi na kimbunga cha maendeleo Zanzibar

**Na Hamid Yassin**

KUELEKEA miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar Januari 12 (keshokutwa) na miaka minne ya Serikali ya Awamu ya nane inayoongozwa na Dk. Hussein Ali Mwinyi, kasi ya maendeleo inaonekana dhahiri shahiri iko juu katika kila pembe ya visiwa vya Unguja na Pemba.

Kwa lugha rahisi, Dk. Mwinyi amejitahidi sana kutekeleza ahadi zake alizotoa wakati akiomba ridhaa ya kuongoza Zanzibar sambamba na kutekeleza kwa kiwango kikubwa Ilani ya Uchaguzi ya chama chake cha CCM.

Kama huamini kwamba uongozi wa Dk. Mwinyi umekuwa neema kubwa kwa Wazanzibari angalia tu wingi wa miradi ambayo imezinduliwa katika kuelekea maadhimishi haya ya Mapinduzi Matukufu na mingine inayoendelea. Ndio maana kumetokea watu hata wakafikiria kuona uwezekano wa kuongeza vipindi vya uongozi Zanzibar kutoka miaka minne hadi saba!

**MIUNDOMBINU**

Agosti 5 mwaka 2022 Dk. Mwinyi alizindua mradi mkubwa wa ujenzi wa barabara Mkoa wa Mjini na kuwataka wananchi kutoa ushirikiano wa dhati wakati wote wa ujenzi ule uliofanywa na Kampuni ya China Civil Engeneering Construction Cooperation (CCECC) kutoka China.

Katika hafla ya utiaji saini wa mradi huo, Dk. Mwinyi aliagiza wananchi waeleweshwe mazingira halisi ya kazi za ujenzi, huku pia akivitaka vyombo vya habari kote Zanzibar kuelimisha jamii juu ya ujenzi huo mkubwa na changamoto zake.

"Naomba wananchi wawe wavumilivu na wastahamilivu wa changamoto zitakazojitokeza wakati wa ujenzi huu mkubwa wa barabara utakapoanza," alisihi Dk. Mwinyi.

Alisema mkataba ule wa ujenzi wa barabara zile ulilenga kuubadili Mji wa Zanzibar, hivyo akazitaka idara za manispaa kuhakikisha zinaweka sheria ndogondogo za utunzaji barabara na maeneo ya hifadhi zake.

Rais Dk. Mwinyi alifafanua kwamba, hakuna nchi yoyote duniani iliyoweza kupata maendeleo bila ya kuwa na miundombinu bora, ndiyo maana Serikali yake iliweka kipaumbele katika uimarishaji wa miundombinu bora ya barabara mjini na vijijini.

Aliongeza kuwa, kipaumbele hicho cha kuing'arisha Zanzibar pia kinahusu maeneo mengine, ikiwemo uimarishaji wa viwanja vya ndege vya Unguja na Pemba, Bandari ya Malindi, Mangapwani na nyinginezo, kuwepo kwa umeme wa uhakika pamoja na matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT) kwa kuzingatia kuwa uchumi wa kisasa umejikita kidijitali.

Alisema Serikali yake ilikamilisha mikataba ya ujenzi wa barabara za mjini na vijijini zenye urefu wa kilometa 200 na akatumia fursa hiyo kuiagiza Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kuhakikisha barabara hizo zinakamilika ifikapo mwaka 2025.

Kutoka mwaka 2022, ikiwa ni miaka miwili nyuma tangu kuapishwa kuwa Rais wa Zanzibar Jumatatu ya Novemba 2, mwaka 2020 mpaka sasa Januari 2024, mbali na suala la kutimiza kwa sehemu kubwa ahadi yake ya ujenzi wa miundombinu, Dk. Mwinyi ameshafanya mengi ya kuijenga Zanzibar yote kwenye miundombinu na masuala mengine bila kubagua Unguja na Pemba!

**UCHUMI WA BLUU**

Mbali na kasi ya ujenzi wa barabara, na miradi mingine lukuki, kumekuwa na uimarishaji wa viwanja vya ndege vya Unguja na Pemba, Bandari ya Malindi, Mangapwani na nyinginezo.

Kuwepo kwa umeme wa uhakika pamoja na matumizi ya ICT, moja ya sera na dira alizoingia nazo Rais Mwinyi wakati wa kampeni zake za urais mwaka 2020 ilikuwa ni kusimamia shughuli zote za uendelezaji na ukuzaji wa uchumi kwa kupitia matumizi bora ya rasilimali zote muhimu za bahari.

Dhana nzima ya uchumi wa bluu ni pana. Imebeba shughuli zote za msingi zinazofanywa katika bahari kama vile, uvuvi wa aina mbalimbali ukiwemo wa kibiashara na usio wa kibiashara katika kina kirefu na kifupi cha maji, shughuli za usafirishaji baharini, shughuli za utafutaji na uchimbaji wa madini na mafuta baharini, kilimo cha mwani na kadhalika.

Rais Mwinyi mara baada ya kuingia madarakani mara moja alianza kuifanyia kazi ahadi yake hiyo kwa kuunda Wizara Maalumu ya Uchumi wa Bluu na kumteua Abdallah Hussein Kombo (wakati huo) kuwa Waziri wa Wizara hiyo. Waziri wa sasa ni Masoud Makame.

Rais Mwinyi amejipambanua yeye na Serikali yake kwamba dhamira ni kujenga Zanzibar mpya kwa kupitia uchumi huo wa kisasa, yaani Uchumi wa Bluu ambao una nafasi kubwa ya kuinyanyua zaidi Zanzibar.

Katika moja ya hotuba zake, Dk. Mwinyi alisema kuwa uchumi wa bluu (ama uchumi wa bahari) unafungamanisha kwa pamoja sekta za uvuvi, ufugaji samaki, ujenzi wa viwanda vya samaki, ukulima wa mwani, uchimbaji wa mafuta na gesi, matumizi bora ya rasilimali mbalimbali za bahari pamoja na shughuli za utalii wa fukwe na michezo ya baharini.

Aliongeza kuwa uchumi wa bluu haukamiliki bila ya kuwepo kwa bandari za kisasa zenye ufanisi wa hali ya juu, hivyo lengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kujenga bandari kubwa za kisasa ambazo zitatoa huduma kwa wavuvi na kuchangia kukuza uchumi.

Dk. Mwinyi aliongeza kuwa, rasilimali za baharini ni moja ya utajiri mkubwa uliopo Zanzibar, lakini bado haujanufaisha nchi na wananchi kwa kiasi kikubwa kama inavyotakiwa, pengine kwa sababu ya kipato kidogo cha wavuvi wa Zanzibar, uwekezaji mdogo katika eneo hilo sambamba na matumizi ya teknolojia duni.

Alisema uvuvi wa bahari kuu ni eneo ambalo limekuwa likiziingia nchi mbalimbali za magharibi fedha nyingi ambazo zinawasaidia kukuza uchumi wao na kuiwezesha serikali kutoa huduma za jamii kwa wananchi wake tofauti na ilivyo kwa Zanzibar.

Ni jambo la kupendeza kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuiona dhana ya uchumi wa bluu kama fursa adhimu itakayoleta mabadiliko ya kiuchumi visiwani humo.

Zipo nchi mbalimbali zilizojikita katika uchumi wa bluu na zimefanikiwa kupiga



## Maendeleo



hatua kubwa kiuchumi.

Katika bara letu la Afrika, nchi ya Afrika Kusini inatajwa kuwa mbele zaidi katika kuendeleza na kutumia dhana ya uchumi wa bluu kama mkakati wake wa maendeleo ya uchumi.

Ni vizuri kwa Zanzibar kujifunza namna ambavyo nchi nyingine zinavyotumia bahari, mito na maziwa kama fursa adhimu ya uchumi si kwa mtu mmoja mmoja tu bali kwa Taifa kwa ujumla.

Sekta nzima ya uvuvi kwa upande wa Zanzibar inatajwa kuchangia asilimia 2.6 ya pato ghafi la Zanzibar ambapo hutoa ajira za moja kwa moja zaidi ya laki mbili ndani ya visiwa hivyo huku zaidi ya watu laki nne wakiwa wanaishi kwa kutegemea sekta hii.

Hakuna ubishi kwamba kuimarika kwa sekta ya uvuvi na matumizi mazuri ya bahari kiuchumi yatachangia kukua kwa uchumi wa nchi pamoja wananchi kwa ujumla.

Kwa mantiki hiyo, kitendo anachofanya Rais Mwinyi kuendelea kuweka mipango iliyo thabiti katika kutekeleza sera yake ya kukuza uchumi kupitia bahari (Blue Economy) haina budi kupongezwa na kuuungwa mkono.

Kitendo kilichofanywa na Serikali cha kuwainua wanawake kwa kuwapatia nyenzo mbalimbali zitakazo wawezesha kumudu shughuli zao za baharini, pia ni cha kupongezwa sana.

Asilimia mbili ya wanawake duniani kote hujishughulisha na shughuli mbalimbali za bahari hivyo Serikali ya Mapinduzi ikiweka mazingira mazuri kwa wanawake hawa katika kujiendeleza na shughuli zao itachangia sana kukua na kukuza sekta ya bahari.

Ili kuwa na uchumi endelevu na kuenda sambamba na mataifa mengine Serikali inapaswa kuwa na mipango imara inayotekelezeka.

Nilifurahishwa na kauli ya Rais Dk. Mwinyi kwamba serikali yake imeamua kuchukua hatua ya kuhakikisha zao la mwani linapata thamani na wakulima wake wanafaidika na kilimo hicho ikiwa ni pamoja na kujenga kiwanda cha kusarifu mwani huko Chamanangwe, kisiwani Pemba ambacho sasa kimekamilika.

### MAHUSIANO KIMATAIFA

RAIS Mwinyi amejenga uhusiano mzuri na nchi mbalimbali duniani sambamba na taasisi kadhaa kubwa duniani. Katikati ya mwaka 2022 aliipongeza Benki ya Dunia kwa kuendelea kuiunga mkono Zanzibar katika sekta mbalimbali za maendeleo.

Dk. Mwinyi alitoa pongezi hizo wakati alipofanya mazungumzo na Makamu wa Rais wa Benki ya Dunia anayesimamia Kanda ya Kusini mwa Afrika, Bi. Victoria Kwakwa aliyekwenda Ikulu ya Zanzibar kwa ajili ya kujitambulisha na kueleza jinsi ya utekelezaji wa miradi iliyo chini ya Benki hiyo.

Katika pongezi hizo, Rais Mwinyi alieleza kwamba Benki ya Dunia ina historia ya muda mrefu katika kuiunga mkono Zanzibar kwenye sekta za maendeleo.

Mwinyi alisema Zanzibar ni miongoni mwa nchi zilizoathirika na Uviko-19 hasa upande wa sekta ya utalii ambayo kwa muda mrefu imekuwa na mchango mkubwa katika pato la Zanzibar.

Hata hivyo, alisema kwamba, shughuli za utalii Zanzibar zimekuwa zikiimarika kila uchao baada ya kupungua kwa kiwango kikubwa cha tishio la janga la Uviko-19, hatua ambayo inapelekea watalii kutoka nchi kadhaa duniani kuitembelea Zanzibar kwa wingi.

Aidha, Rais Dkt. Mwinyi alimweleza kiongozi huyo wa Benki ya Dunia kwamba hatua zilizofikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuendeleza miradi ya elimu na afya inayotokana na fedha za Uviko-19 zilizotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), ili kushughulikia huduma za jamii.

Rais Mwinyi alimweleza makamu huyo wa Rais jinsi Serikali anayoiongoza ilivyoweka kipaumbele na kutilia mkazo uimarishaji wa sekta ya elimu, maji, miundombinu ya barabara pamoja na huduma za kijamii huku akieleza juhudi zinazochukuliwa katika suala zima la kuongeza nishati ya umeme Zanzibar.

Sambamba na hayo, Rais Dk. Mwinyi alimhakikishia Makamu huyo wa Rais wa Benki ya Dunia kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendeleza uhusiano na ushirikiano uliopo kati yake na Benki hiyo hasa kwa kutambua juhudi inazozichukua katika kuiunga mkono Zanzibar kwenye sekta zake mbalimbali za maendeleo.

Tangu wakati huo, Dk. Mwinyi ameshafanya ziara nyingi nje ya nchi katika kuimarisha mahusiano na kukaribisha wawekezaji Zanzibar achilia mbali wale wageni mbalimbali wa mataifa ya nje aliowapokea kwenye Ikulu ya Zanzibar na kupanga nao mikakati mbalimbali ya kimaendeleo.

### MICHEZO

Katika Hotuba yake ya Desemba 27 2023 wakati akizindua Uwanja wa Amani New Complex baada ya ukarabati mkubwa, aligusia suala la yeye kupachikwa majina mengi kutokana na kutekeleza ahadi zake zote alizozitoa mwaka 2020 kwenye kampeni zake wakati alipokuwa akigombea urais wa visiwa hivyo vya Zanzibar.

Alisema watu wanamwita Hussein mabasi, Hussein mabarabara, Hussein maghorofa lakini yeye akawaambia na bado kuna mambo mengi yanakuja ikiwemo hivi karibuni watamwita Hussein Ma-flyover.

Akasema hiyo ni mbali na mpango wa kujenga miundombinu ya michezo kila Wilaya ya Zanzibar kwa viwanja vipya vya kisasa ambao umekamilika.

Aliwapasha Wazanzibari kuwa Serikali yake na na Serikali ya Ujerumani kupitia Shirika la Maendeleo la GIZ imeingia mkataba wa makubaliano ya ujenzi wa viwanja vitano vidogovidogo vya michezo ikiwemo mpira wa kikapu, mpira wa wavu, mpira wa mikono na mpira wa pete.

Viwanja hivyo vitajengwa Kangani Wilaya ya Mkoani, Mchangamdogo Wilaya ya Wete, Tumbatu na Mkokotoni Wilaya ya Kaskazini A na Haile Selasie Wilaya ya Mjini pamoja na viwanja vitatu vya Tenisi Chakechake, Chuo Kikuu cha SUZA Kampasi ya Nkuruma na shule ya Regeza Mwendo katika Wilaya ya Magharibi B.

Mbali na hilo aliahidi kuwa, Serikali yake itajenga uwanja mwingine wa kisasa ambao utatumika katika mashindano ya AFCON ya mwaka 2027 ambayo Tanzania, Uganda na Kenya zitakuwa nchi mwenyeji.


Kasi anayokwenda nayo Dk. Mwinyi katika kutekeleza ahadi zake alizozinadi wakati wa kampeni zake za Urais mwaka 2020, ni ya kupongezwa. Katika kipindi hiki kinachoelekea miaka yake minne madarakani amefanya mambo mengi mazuri si hayo tu niliyoyataja kwenye makala haya, kuna mengi mengineyo.

*Kwa mawasiliano na mwandishi wa makala haya, 0784 122020, O768 888787*



# Vyakula vinne bora kwa kuboresha kumbukumbu





USAHAULIFU ama kupoteza kumbukumbu, ni tatizo linalokua kwa kasi miongoni mwa watu. Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), kuna wagonjwa takriban milioni 50 wa kupoteza kumbukumbu kote ulimwenguni, idadi hii ikitarajiwa kuongezeka mara tatu ifikapo mwaka 2050.

WHO inasema mbali na kumuathiri mgonjwa mwenyewe, ugonjwa wa kupoteza kumbukumbu unaathiri pia familia yake na unaongeza gharama za kiuchumi kwa jamii. Inatarjiwa kwamba ifikapo mwaka 2030, gharama hiyo itafikia Dola trilioni 2 kwa mwaka.

Kwa mantiki hii, ni tatizo ambalo linapaswa kushughulikiwa kwa nguvu zote na kwa sababu hakuna tiba kwa sasa, WHO inasisitiza umuhimu wa kuzuia kutokana na umuhimu wa kumbukumbu katika maisha ya binadamu.

**Aina za Kumbukumbu**

Mwanasaikolojia Kimberley Wilson, anasema ziko aina tatu za kupoteza kumbukumbu, za muda mfupi, ambapo uwezo wa mtu unamfanya kukumbuka mambo yaliyotokea muda mfupi uliopita. Kwa mfano, mtu anakutajia namba ukaipiga bila kuiandika mahali.

Kumbukumbu ya kazi, inayomfanya mtu kuelewa jambo na kuchangia mawazo kwenye mazungumzo yanayoendelea, lakini kumbukumbu za muda mrefu ni zile zinazomfanya mtu kukumbuka matukio ya muda mrefu, hata miaka na miaka.


'Vile tunavyokula, huathiri viwango vya kumbukumbu zetu zinavyofanya kazi', anasema Kimberly.

**Wazee ndiyo waathirika wakubwa**

Tatizo la kupoteza kumbukumbu, linawakumba kwa kiasi kikubwa watu wenye umri mkubwa.

'Ni kweli watu wenye umri mkubwa hasa kuanzia miaka 70, hupata tatizo hili pia, ingawa kwa wengine wenye umri mdogo, wanaweza kulipata ila kwa uchache', anasema Mwajombe Laurian, kutoka Tanzania ambaye ni mwalimu wa kutoa elimu ya lishe kwa afya, ikiwemo kusaidia kumbukumbu.

WHO, Mwajombe na mwanasaikolojia Kimberley, wote wanasisitiza umuhimu wa kushughulikia tatizo hilo na njia iliyo rahisi na kuthibitishwa ni kupitia vyakula.





Miongoni mwa vyakula vinavyosaidia kwenye kumbukumbu ni hivi hapa:-

**1. Zabibu za rangi ya zambarau**

Ziko aina kadhaa za zabibu, ambazo maarufu ni zile zenye rangi ya kijani na za rangi ya zambarau. Watafiti wanathibitisha zabibu za zambarau zina mchango mkubwa kwenye kumbukumbu.

Kwa watu wazima wenye matatizo ya kumbukumbu, wakinywa nusu lita ya juisi ya zabibu za rangi ya zambarau kila siku kwa muda wa wiki 12 (miezi mitatu) zitawasaidia.

Zabibu za zambarau, zina kitu kinaitwa Anthocyanins na Polyphenols vinavyoipa rangi iliyokolezwa ambayo ni muhimu. Polyphenols pia inapatikana kwenye matunda mengine kama apple na mapeasi.

Wakati wa mmeng'enyo wa vyakula hivi baada ya kuliwa, vinasaidia kuifanya mishipa ya damu kunyumbulika vizuri na kutembea kwa damu kuelekea kwenye ubongo.



**2. Blueberries**

'Watoto kula gram 240 (kama robo kilo) ya Blueberries kwa kila siku, huwasaidia kukumbuka maneno mengi na kuyakumbuka kwa usahihi saa mbili baadaye', anasema Kimberley.

Kima ilivyo kwa zabibu za zambarau Blueberries pia zina kitu Anthocyanins na Polyphenols. Kama inavyofanya zabibu kwenye mishipa ya damu, Blueberries pia inaifanya mishipa ya damu kunyumbulika vizuri na kutembea kwa damu kuelekea kwenye ubongo. Hilo linasaidia kuleta nguvu zaidi, virutubishi na oksijeni.

**3. Chocolate**

'Taarifa njema kwa wapenda chokleti ni kwamba huboresha usambazaji wa damu kwenye akili, lakini inapaswa kuwa 'dark chocolate' ambayo ina asilimia 70 ya virutubishi vya kakao (Cocoa solids) ili kupata faida yake', anasema Kimberley.

Lakini wataalamu wanasema muhimu kula mlo kamili wenye mboga za majani, matunda, protini kama samaki na maharage kwa sababu una faida kubwa kwenye ubongo wa mwanadamu.



**4. Grean Tea**

Ukiacha kusaidia kukulinda na saratani, hatari ya kupata magonjwa ya moyo, unene, pia husaidia kuboresha afya ya akili.

Chai hii ina faida kubwa kwenye kumbukumbu. Hasa wenye tatizo la kumbukumbu za muda mfupi, grean tea, inaweza kuwasaidia sana. BBC.

# Ujerumani na China za kwanza kutambua Mapinduzi ya Z'bar



Rais wa Kwanza wa Zanzibar na kiongozi wa Mapinduzi, Abeid Amaan Karume.

Uwanja wa Amaan uliojengwa kwa masaada wa China. Sasa New Amaan Sports Complex

Aliyekuwa Mwenyenyiki wa Jamhuri ya Watu wa China, Mao Zedong.

**Na Mwandishi Wetu**

KESHO kutwa, Januari 12 ni siku adhimu ya kukumbuka Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar yaliyojiri tarehe kama ya keshokutwa, mwaka mwaka 1964.

Hatua ya kumpindua Sultani ndio ilileta uhuru kamili wa Wazanzibari na ni hatua ambayo pia ilisababisha kuwepo kwa muungano wa Tanganyika na Zanzibar tunaojivunia leo uliozaa Tanzania. Baada ya kufanyika kwa mapinduzi hayo, dola kubwa duniani, zipo zilizosuasua kuyatambua lakini zipo zilizoyaunga mkono mara moja na kuahidi kusaidia maendeleo ya wananchi wazalendo wa Zanzibar katika kuanzisha miradi mbalimbali ya maendeleo.

Ushawishi wa mapema ulijitokeza katika kila kundi ambapo kwa wakati ule Zanzibar ilikuwa na uhusiano wa karibu na nchi za Urusi, Ujerumani ya Mashariki pamoja na Cuba. Kwa mujibu wa vyanzo mbalimbali vya uhakika, Mapinduzi ya Zanzibar yalitambuliwa kwa mara ya kwanza haraka na nchi mbili ambazo hazikuishia tu kuyatambua bali pia kuchukua jukumu la kusaidia maendeleo ya wazalendo.

Nchi hizo ni China, iliyokuwa Ujerumani Mashariki, Cuba pamoja na Urusi ambapo katika kipindi cha harakati za ukombozi za Wazanzibari kudai uhuru, tayari vijana wa Chama cha Afro Shirazi walikuwa wakipelekwa katika nchi hizo kwa ajili ya mafunzo mbalimbali yakiwemo ya kijeshi.

Moja ya misaada iliyotolewa na nchi hizo ni wataalamu wakiwemo wa kijeshi katika vikosi vya ulinzi, usalama wa taifa na kikosi cha wanamaji cha KMKM.

Hadi kufikia Aprili 26 mwaka huo huo wa 1964 ambapo Zanzibar iliungana na Tanganyika na kuzaliwa kwa taifa jipya la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tayari nchi 18 zilikuwa zimeyatambua mjapinduzi hayo.

Nchi tisa zilifungua ofisi za ubalozi kamili Zanzibar ambazo ni Marekani, Urusi, Ujerumani Mashariki, China, Uingereza na kwa Afrika nchi ya kwanza kufungua ubalozi wake Zanzibar ilikuwa Ghana. Nchi hiyo ya Afrika Magharibi iliyuatambua mapinduzi hayo tarehe 28, Januari, 1964 na baadaye kufungua ubalozi kamili. Hata hivyo, baada ya kuzaliwa kwa muungano, ofisi hizo zilifungwa na nyingine kubaki balozi ndogo.

Sababu zilizoifanya Ghana kuyatambua mapema Mapinduzi ya Zanzibar ni uhusiano wa asili wa viongozi wakuu wa nchi hiyo na Tanzania katika kupigania uhuru akiwemo Mwalimu Nyerere, Karume pamoja na Kwame Nkrumah.

Ikimbukwe pia kwamba Ghana ilikuwa nchi ya kwanza katika Bara la Afrika kupata uhuru wake kutoka kwa Muingereza mwaka 1957 ambapo Rais Kwame Nkrumah aliwaalika baadhi ya viongozi wa nchi za Afrika kuwapa mbinu na ujanja wa kudai uhuru.

Miongoni mwa walioalikuwa alikuwa Rais wa Kwanza wa Zanzibar aliyeongoza mapinduzi hayo, Sheikh Abeid Aman Karume.

Aidha inaelezwaa kwamba mikutano ya wapigania uhuru wa Afrika Mashariki na Kati (Pan-African Freedom Movement of East and Central Africa-PAFMECA) kwa kiasi kikubwa ilisaidia kuwakutanisha viongozi hao ambao kwa wakati huo walikuwa katika harakati za kupigania uhuru.

Taarifa zinaonesha kwamba viongozi wa Afrika hasa Mwalimu Nyerere, Kwame Nkrumah wa Ghana na Abeid Amaan Karume wa Zanzibar walikuwa na mawazo ya pamoja ambayo lengo lake ilikuwa ni kuhakikisha kwamba bara la Afrika linakuwa huru na kwa wakati ule Nkrumah alikuwa na mwelekeo wa mapema katika kupiga vita harakati za ukoloni wa Kiingereza. Pia viongozi hao walikuwa na maono ya kuunganisha nchi za Afrika kuwa nchi moja.

Rais Nkrumah katika kuwaunga mkono wana wa Afro Shirazi Party (ASP) alimleta wakili Swanzi kwa ajili ya kuwatetea wanachama wa ASP ambao walishtakiwa kwa mauaji katika fujo zilizotokea Juni mwaka 1963.

Kuanzia hapo marais na viongozi wakuu wa nchi mbalimbali duniani walikuwa na hamu kubwa ya kuitembelea Zanzibar na kujionea harakati zake za kupigania uhuru.

Miongoni mwa viongozi mashuhuri waliotembelea Zanzibar alikuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Watu wa China wakati wa uongozi wa Mwenyekiti Mao Tsetung (au Mao Zedong kwa lahaja inayotumika sasa China), Chou En Lai (Zhou Enlai) ambaye alizuru Zanzibar tarehe 5/6/1965.

Alipofika uwanja wa ndege wa Zanzibar na kulakiwa na Rais wa Zanzibar, Abeid Amaan Karume na Makamu wa Pili wa Rais wa Tanzania, Rashid Mfaume Kawawa.

Wengine waliozudu Zanzibar mpya walikuwa ni Rais wa Liberia, William Tubman, Mfalme Haille Selassia wa Ethiopia, Rais wa Misri, Gamal Abdell Naser na Rais wa Yugoslavia, Broaz Tito.

Ujerumani Mashariki ilisaidia ujenzi wa kwanza wa nyumba za maendeleo za kupigiwa mfano zilizopo Kikwajuni Zanzibar, ambazo mafundi wazalendo walipata ujuzi uliosaidia kujengwa kwa nyumba nyingine za maendeleo ziliopo Michenzani, Kilimani na sehemu nyingine za vijijini na Pemba.

Kadhalika, kumbukumbu zilizopo zinaonesha kwamba Ujerumani walileta meli kubwa ambayo ilibeba kila kitu kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya Kilimani ikiwemo saruji na vifaa vingine. Kadhalika waliipa Zanzibar misaada ya vifaa mbalimbali kwa ajili ya kikosi cha majini cha KMKM.

China kwa upande wake ilisaidia maendeleo ya Zanzibar kwa kujikita zaidi katika kusaidia ujenzi wa viwanda mbalimbali vya uzalishaji wa bidhaa, kikiwemo kiwanda cha ngozi na viatu kilichopo Maruhubi.

China pia ilisaidia ujenzi wa kiwanda cha Sigara, kiwanda cha sukari kilichopo Mahonda kwa ajili ya kupunguza tatizo la kuagiza bidhaa hiyo nje ya nchi.

China pia inatajwa kusaidia ujenzi wa kiwanja cha mpira cha Amaan ambacho katika miaka ya 1972 kilikuwa ndicho kiwanja kikubwa katika ukanda wa Afrika ya Mashariki na Kati. Kiwanja hicho kilifunguliwa na Mwalimu Nyerere mwaka 1971.

Katika kuelekea miaka 60 ya mapinduzi, Serikali ya Awamu ya Nane inayoongozwa na Rais Dk. Hussein Mwinyi imekikarabati vyema kiwanja hicho kwa awamu ya tatu kwa viwango vya kimataifa ambapo sasa kinaitwa New Amaan Sports Complex.

Kwa kipindi kirefu, China pia imekuwa ikiisaidia Zanzibar madaktari katika fani mbalimbali ambao huenda Zanzibar kufanya kazi. Madaktari hao walianza kuja Zanzibar mwaka 1965 na kuanza kusaidia kutoa tiba kwa wananchi wa Zanzibar. Wakati huo madaktari bingwa wazalendo walikuwa watano tu.

Utaratibu wa madaktari bingwa wa China kuja Zanzibar umekuwa ukiendelezwa ambapo madaktari hao wapo katika hospitali zote kuu za Unguja na Pemba.

Mwandishi wa kitabu cha historia ya Abeid Amaan Karume na Mapinduzi ya Zanzibar, Ali Shaaban, anasema katika kitabu chake kwamba Mapinduzi ya Zanzibar yalizusha mivutano kwa mataifa makubwa huku kila mmoja akitaka 'kujipendekeza kwa Zanzibar' na kukubalika

Shaaban anasema, hata hivyo, Karume aliliona hilo mapema na kuchukua tahadhari ambapo katika juhudi za kukata mzizi wa fitina alitangaza kufungwa mara moja kwa kituo cha upelelezi cha kijeshi cha Marekani kilichokuwa Tunguu wilaya ya kati Unguja.

Kituo hicho kilichojulikana kwa jina la "Mercury project" kwa ajili ya mawasiliano ya anga za juu kilifungwa rasmi Aprili 7, mwaka 1964.

Aidha Karume alitangaza kufukuzwa kwa Balozi wa Marekani nchini Zanzibar, Frank Calucci na Ofisa wa Ubalozi Robert Gordon Februari 16 mwaka 1964 ambao walituhumiwa kufanya njama za upelelezi na kutaka kuipindua Serikali halali ya wananchi wa Zanzibar ikiongozwa na Karume.

"Hayo ni sehemu ya maamuzi mazito yaliyochukuliwa na Rais Karume kwa taifa kubwa la Marekani ambapo pia akitangaza Zanzibar kujiunga na Umoja wa nchi zisizofungamana na upande wowote," anasema Shaaban katika kitabu chake.



# Kurunzi

Na Dk. Reubeni Lumbagala | 0620 800 462

# Kinana umenena vyema, viongozi 'msifikiri' kwa niaba ya wananchi

HARAKATI za kila siku anazofanya binadamu zina lengo la kuboresha maisha yake na kujiletea maendeleo kwa ujumla. Mkulima shambani, mvuvi baharini, daktari wodini, bodaboda barabarani, mwanafunzi shuleni na wengine wengi, wanafanya juhudi kubwa za kutekeleza majukumu yao ili maisha yaende na hivyo kuchangia maendeleo yao wenyewe na taifa kwa ujumla.

Maendeleo yenye tija ni yale yanayogusa maisha ya watu. Maendeleo yasiyogusa maisha ya watu hayana umuhimu kwa watu. Maendeleo ya watu yanapaswa kutangulia kabla ya kuelekea kwenye maendeleo ya vitu. Maisha ya watu yakiwa bora, hata maendeleo ya vitu yakifuata yatakuwa na maana kubwa.

Ajenda ya wananchi popote pale iwe ni nchi zilizoendelea au nchi zinazoendelea kama Tanzania ni kupata maendeleo yanayogusa nyanja zote za maisha yao, iwe kisiasa, kijamii na kiuchumi. Kiufupi, wananchi wanataka maendeleo tena maendeleo yanayogusa maisha yao moja kwa moja.

Baadhi ya vitabu vya dini vinaonesha kwamba mtu anayependeza sana mbele za Mungu ni yule ambaye jamii kubwa inanufaika naye. Kwa muktadha huo, viongozi wa ngazi mbalimbali, wana nafasi kubwa ya kupendwa na Mungu kwa sababu wana kila sababu ya kuwanufaisha watu wengi.

Mwalimu Nyerere alipata kusema kwamba ukiwa kiongozi mahala, basi ujue madhila ya watu unaowaongoza ni mzigo wako. Ni viongozi wangapi wanatilia maanani hilo?

Viongozi na wananchi kwa pamoja ni wadau muhimu wa kufanikisha azma ya kupata maendeleo. Pande hizi mbili zinapaswa kushirikiana kikamilifu ili kufanikisha na kurahisisha mzunguko wa kasi wa gurudumu la maendeleo. Mipango ya maendeleo inapaswa kuratibiwa kwa karibu kupitia ushirikiano baina ya viongozi na wananchi.

Viongozi hasa wa kuchaguliwa huwa wanaomba ridhaa kutoka kwa wananchi kupitia utaratibu uliopo wa uchaguzi, uwe uchaguzi wa serikali za mitaa au uchaguzi mkuu. Katika kipindi cha uchaguzi, wagombea, hujinadi kupitia majukwaa wakiomba ridhaa ya kuongoza (kwa maana ya kuwawakilisha) kwa kipindi cha miaka mitano na kuahidi mambo mbalimbali ambayo kama wakipata ridhaa watayatekeleza ili kuleta ustawi wa maisha ya wananchi. Ni wawakilishi kwa sababu haiwezekani wananchi wote tukaende Bungeni ili kuisimamia serikali na kutunga sheria. Tunatuma wawakilishi.

Hata viongozi wa kuteuliwa, wana dhima ileile ya kumwakilisha rais tuliyemchagua ama kiongozi aliyewateua kwetu na hivyo bado matatizo ya wananchi ni mzigo wao.

Deni kubwa walilonalo viongozi baada ya kupata dhamana ya kuongoza ni kutekeleza ahadi zao ambazo huwa zina lengo la kuboresha maisha ya wananchi.

Utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo utakuwa na tija kwa wananchi endapo wananchi hao watashirikishwa kikamilifu na viongozi hawa kwa kutoa maoni yao kuhusu nini wangependa kitangulie kutekelezwa katika maeneo yao. Hivyo basi, ni muhimu sana wananchi wakashirikishwa kabla ya kuanza kutekelezwa kwa miradi mbalimbali ya maendeleo ili miradi hiyo ya maendeleo iwe na tija kubwa katika maisha ya kila siku ya wananchi.

Akizungumza na wanachama wa Chama cha Mapinduzi (CCM) na wananchi wa Jimbo la Mtama mkoani Lindi baada ya kuzindua Shina la Chama, Majengo Sokoni, Makamu Mwenyekiti Taifa wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Abdulrahman Kinana ametoa rai kwamba mambo ya msingi yanayohusu maendeleo ya wananchi, ni vyema wananchi washirikishwe kwanza na yatokane na wananchi wenyewe.

Kinana alitoa mfano hai juu ya hoja yake ya kuwashirikisha wananchi kwenye ajenda ya maendeleo. Alieleza kuwa alipokuwa Katibu Mkuu wa CCM akiwa na Nape Nnauye (aliyekuwa Katibu Mwenezi wakati huo) walikwenda wilayani Ngorongoro ambako walifanya mkutano mkubwa.

"Tulipokuwa pale, ukitazama pale kwa mimi ungeniuliza ningesema wale wananchi wanahitaji maji, lakini tulipowauliza wenyeji, wakasema tatizo lao si maji bali ni mtandao wa simu. Unaweza ukaona wewe unakwenda mahali ukifikiri shida ya watu ni shule, ni maji kumbe shida yao ni jambo lingine kabisa ndiyo maana ni lazima tuwashirikishe wananchi," alisema Kinana.

Hii pia imenikumbusha kwamba kuliwahi kuwepo matukio ya baadhi ya halmshauri kujenga masoko na kisha yakabaki kama magofu kwa sababu wananchi waliyatekeleza, wakawa wanaendelea kutumia 'masoko mjinga'. Hii yote ilitokana na wakubwa wa halmashauri 'kufikiri kwa niaba ya wananchi' badala ya kuwashirikisha wananchi ni wapi mahala sahihi pa kujenga soko.

Mfano hai ni pale Musoma Mjini ambapo Halmashauri ya Mji (wakati huo, miaka ya 1980) ilijifungia kibwebwe kuwaamlia wananchi kujenga soko la kisasa na kubwa katika eneo la Kamunyonge lakini wananchi walilitelekeza na kufanya manunuzi yao kwenye soko mithili ya genge wakati huo la Nyasho ambalo lilikuja kuendelezwa baadaye!

Kutokana na viongozi kuwa na jukumu la kuboresha maisha ya wananchi wao, juhudi zao zitaleta matunda na hata kuwa na uhakika wa kuchaguliwa tena endapo viongozi wataibua na kutekeleza miradi inayogusa maisha ya watu. Vivyo hivyo kwa viongozi wa kuteuliwa, mamlaka za uteuzi kila mara zitawafikria pale watakapokuwa wanafanyia kazi kwanza matakwa na maslahi ya wananchi.

Hata kama viongozi ni wakazi wa maeneo hayo, ni muhimu wawashirikishe wananchi wao juu ya miradi gani itangulie kutekelezwa ili miradi hiyo iwe na tija kwa wananchi kwa wakati huo.

Si jambo lenye afya kwa kiongozi kudhani kuwa anajua kila kitu, hivyo kuchukua jukumu la kupigia debe utekelezwaji wa miradi ya maendeleo kadri anavyofikiria yeye bila kupata ushauri na pengine ridhaa kutoka kwa wananchi wake.



Changamoto zinaweza kuwa nyingi katika eneo fulani la utawala; mathalani, kijiji hakina zahanati, shule, maji, umeme, stendi na kadhalika.

Ikiwa hakuna fedha za kutosha za kumaliza changamoto hizi kwa wakati mmoja, ni muhmu kwa viongozi kuwashirikisha wananchi juu ya mradi gani uanze kutekelezwa kutokana na uzito wake kwao.

"Katika kuamua mambo yanayohusu maisha yao, tusichukue amana ya kuwafikiria, tusichukue mamlaka ya kuwaamulia. Ni vizuri tukae na wananchi tuzungumze nao ili watuambie kitu gani wanakihitaji kwa wakati gani na kwa sababu gani," amesema Kinana.

Mwangi wa hili alilolisema Kinana ni vyema ufike hadi bungeni kwa maana ya wawakilishi hao wa wananchi kufanya mikutano kwa wingi majimboni ili wawe wakipeleka mawazo ya wapiga kura na si 'kujiwakilisha' wenyewe kwa kusema wanayofikiri!

Vivyo hivyo madiwani ambao ni wawakilishi wa wananchi wa kata zao wanapaswa pia kufanya mikutano mingi na wananchi na kupeleka mawazo yao kwenye vikao vya kupanga maendeleo ya halmashauri. Kwenye mikutano hii, madiwani na hata wabunge wasijitishwe jukumu la kuhutubia wananchi bali wawaache wananchi kuwa wazungumzaji wakubwa ili kusikia sauti zao, kero zao, hoja zao na hata makemeo yao.

Muda umebaki mfupi kabla ya kufanyika kwa uchaguzi mkuu. Unaweza kufanya uchunguzi na kugundua kwamba ni wabunge wachache ambao wamefanya mikutano ya kutosha na wananchi na kusikia kero na mawazo yao. Wapo wabunge ambao wanaonekana tu wakati wa uchaguzi baada ya hapo wanapotea. La kujiuliza, wabunge kama hawa wanamwakilisha nani?

Ni muhimu kwa viongozi wote kuzingatia hili alilosisitiza Kinana juu ya maendeleo ya wananchi. Hata tunapoelekea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu na uchaguzi mkuu mwakani, ni muhimu kwa wagombea kujua kile wananchi wanataka. Kwa kufanya yale wananchi wanataka, hayo ndiyo maendeleo halisi na ndipo kwenye utatuzi wa kero za wananchi na hatimaye kufikia maendeleo ya kweli ya nchi yetu kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

Wapiga kura pia tusichague viongozi 'wanaojiwakilisha' wenyewe, wabinafsi na wasiokaribu na wananchi. Kama ni hundi, basi tunaenda kupewa hundi nyeupe tuandike fedha tunazotaka. Tuwe makini tutakapokuwa tunajaza hiyo hundi.

Kama ambavyo huwa anasema mwanamajumui Profesa Patrick Lumumba, tusinunue pikipiki wakati wa uchaguzi, halafu tukategemea ije ifanye kazi mithili ya Benzi!



Paul Mng'ong'o

## KLINIKI YA FIKRA

Simu: 0676055444 Email: mngongopaul@yahoo.com

# Misumari ya mahusiano - 1



KARIBU tena kwenye kona yetu hii ya kuboresha fikra. Wiki iliyopita tulimaliza kuangalia mada iliyoeleza kwamba watu wenye kujitambua kuna mambo ambayo huwa hawafanyi ng'o.

Tukasema kujitambua si tu kuwa mwerevu, bali pia ni kufanya maamuzi sahihi na kuepuka tabia zitakazokusambaratisha. Bila shaka mambo ambayo hutakiwa kufanya yako mengi lakini baadhi ya hayo kwa kukumbushana tu pamoja na haya:

Kwamba wanaojitambua hawaachi kujifunza, hawakubaliani na mambo tu kirejareja, haiwaingii kwenye magomvi au mabishano, hawazungumzi bila kufikiri kwanza na pia tukaona kwamba wanaojitambua hawakaribishi mtazamo hasi.

Mambo mengine ni kwamba wanaojitambu hawajipi majukumu ya kubadilisha mambo wasiyoyaweza, hawaogopi changamoto, hawasahau kuona picha sahihi, hawashambulii kwa ghadhabu na mwisho hawabakii katika mazungumzo yasiyo na maana.

Leo tumeanza mada mpya kama inavyosomeka hapo juu. Karibu tuendelee nayo.

### 1. KUKUBALIANA (ACCEPTANCE)

Kila mwenzi anahitaji kukubalika kwa mwenzi wake vile alivyo na si kuwa vile ambavyo mwenzi wake anataka awe. Tatizo kubwa ni kwamba tunakutana na wenzi ambao tunataka wawe tunavyotaka na hatuwakubali vile walivyo. Ili kuepuka kulaumiana na kero, mkubali mtu kama alivyo.

Kama umempenda na umemchagua, jukumu lako ni kuthamini yale yaliyokuvuta kwake. Hakikisha unaenda kwa mtu ambaye asilimia ya vitu vya kumkubali ni kubwa kuliko asilimia ya vitu unavyotaka abadilike.

Hakuna siku tutapata wenzi wakamilifu kwa asilimia zote. Kama ukimkubali na kumchagua natumaini kuwa tayari umepata mengi kwake ya kumkubali kuliko ya kumbadilisha na hapo anachokihitaji zaidi ni kukubaliwa.

Mpe uhuru wa kuwa yeye mwenyewe uwapo naye. Najua ni ngumu, lakini jifunze kukubali mapungufu yake na kumkubali. Kisha, unaweza kumhimiza abadilike hatua moja baada ya nyingine. Lakini kumkubali kwanza, kunaweza kumsaidia kubadilika kuliko kuwekeza nguvu kwenye kumbadilisha kabla ya kumkubali.

Kukubalika ni hitaji la msingi zaidi kwa mwanaume. Mwanaume hapendi kurekebishwa sana, kuongelewa maneno ya kero za kumtaka awe mwanamke anavyotaka. Maneno mengi na kero vinampeleka mbali zaidi mwanaume.

Tafiti zinaonesha kwamba wanaume wanapenda sana mambo mawili kwenye mahusiano; kuheshimiwa na kupata furaha kwa mwenza. Kwa hiyo ni vyema wanawake kuwakubali wanaume jinsi walivyo mintarafu mambo hayo mawili.

### 2. KUZINGATIWA (ATTENTION)

Hii ni muhimu kwenye mahusiano. Inatoa ujumbe na ishara kwa mwenzi kwa haraka kuwa yeye pekee ndiye anayependwa na kuthaminiwa zaidi. Mambo kama kumpigia simu, kumwandikia ujumbe wa maandishi, kutumia picha yake kama picha yako ya mbele (screen saver) kwenye simu, laptop, nk vitamwambia mwenzi yeyote kuwa "Nakupenda na ninakuthamini."

Mwenzi anahitaji kutambuliwa, anataka uzime runinga ili uzungumze naye. Anataka kujua kwamba yeye ni wa muhimu zaidi kwako.

Lakini pamoja na maelezo haya, ni muhimu ijulikane kuwa, kuzingatiwa (attention) ni hitaji la msingi zaidi kwa mwanamke kuliko mwanaume.

> Mwanamke akikosa hali hiyo kwa mwanaume wake, mahusiano kwake yanakuwa mepesi na wakati wowote yanaweza kuingiliwa. Hivyo mwanaume unahitajika kuwa imara, jasiri na shujaa.

### 2. UZURI / UREMBO (BEAUTY)

Kwenye mahusiano, daima jitahidi kuwa na mwonekano wa kuvutia kwa ajili ya mwenzi wako. Tunza nywele zako, jali ngozi, punguza uzito unaokithiri, vaa vizuri, nk. Wengi wanaweza kulichukulia poa jambo hili, lakini ni msingi wa mahusiano.

Kila mwenza anatamani kujivunia mwonekano nadhifu na wa kuvutia wa mwenzi wake. Ni vyema ukajali mwonekano wako sababu ni kitu cha thamani kwa mwenzi wako.

Pamoja na kuwa jambo hili ni muhimu kwa wote, lakini ni jambo muhimu na lenye thamani kubwa kwa mwanaume kuliko mwanamke. Wanaume wanavutiwa zaidi na kuona wakati mwanamke anavutiwa sana na mambo yenye hisia.

Kwa hiyo ni muhimu wanawake wakazingatia jambo hili bila kulizidisha. Kuna wanawake ambao wanajali mwonekano mpaka wanazidisha. Wanajipamba kupitiliza hata kuiondoa asili yao kwa "make ups" na vito. Ni vizuri pia kutambua kuwa, mwanaume havutiwi sana na urembo uliokithiri na usio wa asili. Hata kama unaongezea vitu, viwe vinavyoboresha uasilia wako na siyo kuondoa uasilia wako na kukufanya kuwa kitu kingine.

### 3. USALAMA / USHUJAA (BRAVE)

Moja kati ya misingi muhimu kwenye mahusiano ni usalama. Mwenzi anahitaji kujihisi kuwa salama zaidi akiwa kwako kuliko akiwa nje yako. Suala hili linajengwa, ndiyo maana naongea nawe kupitia makala hii.

Jambo hili ni la muhimu zaidi kwa mwanamke kuliko kwa mwanaume. Mwanamke anahitaji usalama wake akiwa na mwanaume, anahitaji kulindwa, anahitaji kujua kuwa atakula, atatibiwa, atavaa, atapendeza na kuonekana wa maana, hatachekwa, atathaminiwa, atalindwa na maswaibu (migogoro) ya familia, hahitaji kuwa na wasiwasi.

Mwanamke akikosa hali hiyo kwa mwanaume wake, mahusiano kwake yanakuwa mepesi na wakati wowote yanaweza kuingiliwa. Hivyo mwanaume unahitajika kuwa imara, jasiri na shujaa.

Mwanamke havutiwi na mwanaume mwoga na dhaifu. Maeneo pekee ambapo mwanaume anahitaji kulindwa na mwanamke ni kwenye hisia zake na kulindwa kwa maombi.

Mwanamke hakikisha mumeo ana amani wakati wote. Mpe pumziko kiasi kwamba hata akipata mishale huko anajua pumziko na faraja ni kwa mwenzi wake. Usiwe na maneno ya karaha na kuhitaji mambo mengi, kuwa msaidizi mzuri na tambua kuwa mwanaume anahitaji mno maombi ya mke wake kwa Mungu.

Wework Consult - Your Partner in Growth.

Itaendelea...



Na Hamisi Kibari

Mtanzani wa kwanza kushinda Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu

# Niko tayari kwa kifo - 15

**Baada ya kuthibitishiwa na daktari kwamba mkewe amefariki dunia kutokana na kipigo alichomshushia, Chris anashirikiana na daktari kuficha kifo cha mkewe akidai ametoweka na hajui alipo. Anaahidi kumsaka. Daktari anaahidi kushughulikia kila kitu na kuondoa katika makabrasha yote hospitalini jina la mkewe. Hata hivyo, gharama za kufanikisha hilo ni kubwa na zinasababisha daktari atwae nyumba ya Chris. Mwanaume huyo ambaye biashara yake ya kuuza mbao na vifaa vya ujenzi ilikuwa inakwenda vyema ghagla inachungulia kaburi. Haya yote ni tangu alipokutana na mrembo aliyekuwa akitikisa mji wa Tabora, Joyce na kuanzisha uhusiano naye. Baada ya kumfilisi, Joyce anamkataa Chris na kugeukia kwa mwanaume mwingine na kusababisha Chris afanye fujo kubwa ya kumpinga Joyce na huyo mpenzi wake mpya na sasa anatafautwa na polisi... Endelea.**

"Shikamoo Mzee Mahmoud," Mwalimu Misango alimsalimia mzee huyo mwenye mchanganyiko wa damu ya Kiarabu na Kibantu. Alikuwa Mzee maarufu mjini Tabora."Marahaba, karibu.""Samahani, nilikuwa ninamuuliza huyu mpangaji wako, Chris Magati. mbona banda halina uhai?"

"Ah! Ni yule dada yake... Nilianza kukusahau mwalimu. Uzee unakuja kwa kasi."

"Ni Mimi baba.""Nina muda mrefu simwoni na sina habari yoyote kutoka kwake. Mimi binafsi ninamtafuta sana. Ninaumwa na hajanilipa kodi miezi sita sasa... Nilidhani wewe dadake ungenisaidia kujua aliko?""Sijui alipo. Ina maana huna tetesi zozote kuhusu mahala alipo?""Tena ningepajua ingekuwa vyema... Kitu kingine ni kwamba huyu kijana sijui kafanya nini huko. Toka wiki iliyopita askari polisi wanakuja kumtafuta hapa mara kwa mara. Anauweka huu mtaa katika msukosuko mkubwa. Watu wananiuliza maswali nashindwa hata kujibu. Kwani kafanya nini huko?""Hata mimi sijui. Nimesikia polisi wakimtafuta ndio maana na mimi nimekuja hapa kuona kama nyinyi mna habari zake zozote.""Mimi sina habari yoyote kuhusu mdogo wako... Tena mwezi huu ukiisha bila kumwona, nitaomba kibali cha polisi, nivunje duka lake nipangishe mtu mwingine na kushika mali zake kufidia gharama zangu ingawa naona kafilisika. Hata sijui kama kuna kitu cha kufidia kodi yangu ninayodai.""Haya baba mimi ninakwenda.""Sawa, lakini ikiwa utamwona, mpe hayo maelezo yangu. Mwisho wa mwezi ninavunja kisha naleta mpangaji mwingine.""Sawa baba," Mwalimu Misango alijibu akiondoka. Aliamua kwenda nyumbani kwa binti aliyekuwa akimuuzia Chris duka, Diana Masemele ili kuona kama anaweza kupata habari zozote kuhusu mdogo wake. Mwalimu alikuwa amejaribu mara kadhaa kumtafuta binti huyo kwa namba ya simu aliyokuwa nayo lakini ilionekana kama haitumii tena.

Hata hivyo, alikuwa hakumbuki vizuri nyumba aliyokua akiishi. Kwa kuwa alikuwa akijua mtaa, Buzebazeba, aliitafuta huku akiulizauliza na kufanikiwa kumpata akiuza genge nje ya nyumba yao.

"He! Siku hizi umefungua genge ama unamuuzia mama yako?" Aliuliza Mwaimu Misango."Ndio, nimefungua genge... Karibu sana, mwalimu. Unadhani nitaendesha vipi maisha yangu kama sikujishughulisha na biashara kama hizi!""Vipi kumetokea nini. Mbona banda la biashara mmefunga?""Mwalimu usin'chekeshe. Yaani unaniuliza mimi kuhusu banda wakati nina karibu mwezi sasa nikiwa sijui kinachoendelea huko? Mara ya mwisho si ulikuja nikakueleza namna hali ilivyo mbaya nikadhani utamweka chini mdogo wako lakini hali ikazidi kuwa mbaya. Kulikuwa hakuna tena cha kuuza pale bandani.""Sijawahi kukutana naye na sina habari kabisa na mahala alipo. Mwanzoni alikuwa hapokei simu yangu lakini sasa namba za simu zake zote nilizo nazo inaonekana kama kabadilisha. Ni kama wewe, tangu majuzi ninakutafuta lakini sikupati kwenye simu.""Simu yangu ilipotea. Nimepata nyingine lakini nimerejesha line moja tu nyingine sijaresha na nadhani ndio ambayo ulikuwa nayo. Kimsingi, biashara ilishindikana baada ya mali bandani kuisha kabisa. Kama nilivyokuelekeza siku ile, mdogo wake na yule mwanamke kila siku wanachukua pesa tu na kwenda kutumbua. Kila nikiuza jioni pesa yote inaondoka. Hakuna mali mpya inayoingia. Hapo kuna biashara tena? Na siku ile nilisita tu kukuambia lakini ninadai mishahara ya miezi mitatu. Siku za mwisho nilikuwa ninasaidiwa kuendesha maisha na mchumba wangu. Ninafikiria kufungua kesi kumshitaki mdogo wako nidai ujirfa wangu."

"Duh! Pole sana Diana… Yaani!"

"Mwalimu, nimeendesha maisha kwa shida sana huku mdogo wako akitumbua tu pesa na huyo hawara yake. Tuseme mkewe ndio kamkimbia kabisa?"

"Mkewe tangu ametoweka hajulikani alipo. Hata mimi nimeanza kuwa na wasiwasi ingawa nilimsikia mara kadhaa akisema anaweza kuamua kumlipizia kisasi mumewe kwa maana na yeye kutafuta bwana. Tena alikuwa akisema bila kunificha kwamba mabwana wanaomtaka, hadi wengine kumshawishi aachuke kwenye ndoa ili wamuoe hata kama keshazaa wako wawili. Mimi nikawa ninamwambia wanakudanganya tu. Hayo mawazo kwamba anaweza kuwa kafuchwa na bwana sasa yametoweka kwa sababu hii sasa si kawaida. Yaani imekuwa shida juu ya shida. Sasa ni zaidi ya miezi nane na mimi ndiye ninayehangaika na watoto wao. Nilijua pengine unajua mahala alipo.""Kwa kweli sijui.""Haya Diana, Kwa heri," alisema Mwalimu Misango akiondoka kinyonge.

***

Mwalimu Misango alimpakata Huba ambaye alikwenda kumshitakia huku akilia baada ya kukorofishana na kaka yake Kenny, wakati wakicheza jioni hiyo.

Mwalimu alihisi Huba ameanza kupata joto baada kupitisha kiganja chake cha mkono wa kulia kwa nyuma kusikiliza joto la mtoto huyo ambaye alikuwa akiendelea kulia. Usiku ulioipisha usiku Huba alilala na homa, Mwalimu akampa dawa za kutuliza maumivu lakini kulipokucha asubuhi, na hadi Mwalimu anakwenda kazini, mtoto huyo wa miaka mitatu na nusu alikuwa anaendelea vizuri.

Licha ya msichana wa kazi kumjulisha kwa simu kwamba Huba alikuwa anaendelea vizuri akicheza kama kawaida, Mwalimu Misango aliomba ruhusa mapema kazini ili kuja kuangalia maendeleo ya hali yake.

Tofauti na mchana wakati anafika, sasa joto lilianza tena kupanda.

"Nyamaza Huba, nitamchapa Kenny kwa uchokozi," alisema Mwalimu Misango akipanga kumpigia mumewe simu asipitie kokote jioni hiyo akitoka kazini ili wampeleke hospitali Huba.

"Mtoto analia nini, au amemkumbuka mama yake. Bado hajazoea tu?" Alihoji mumewe ambaye alikuwa anaingia nyumbani jioni hiyo akitokea kazini.

"Kachokozana na kaka yake. Kimsingi Huba ameanza kumsahau mama yake... Isipokuwa ameanza kuchemka tena. Nilikuwa ninapanga kukupigia simu ili uwahi tumpeleke hospitali jioni hii."

"Sawa. Yaani mama mtu ameamua kuuchuna kabisa huko aliko? Mama gani unatelekeza watoto ili kulipa kisasi kwa mume wako?"

"Hilo nalo nilitaka tulijadili Baba Kessy. Hali hii si ya kawaida. Kwa nini mama mtu kama bado yuko hai asimkumbuke mwanae?" Alihoji Mwalimu Misango. Mumewe aliyekuwa amesimama karibu yake akabaki kimya.

Mwalimu akaendelea: "Hata baba mtu, hapo nyuma ukiona katuma meseji ni ya kuuliza watoto wake. Ukiona katuma pesa ni kusaidia malezi ya wanawe, naye miezi miwili sasa kimya. Hajulikani alipo, simu zake hazipatikani wala nini. Si Hali ya kawaida na hatuwezi kubali kimya."

"Unashauri tufanyeje?"

"Kinachonishangaza hata Jacob na baba yake mdogo wamekaa kimya. Mara ya mwisho nilipoongea na Jacob kumjulisha yaliyomkuta shemeji yake, majibu yake kidogo yalinishangaza. Alisema wao sasa wamemwachia Mungu hawataki kupoteza muda wala kusikia kabisa habari za Baba Kenny. Majibu gani hayo sasa?"

"Hujajibu swali langu. Tufanyeje?"

"Nilikuwa nashauri twende polisi kutoa taarifa kuhusu kupotea kwa Baba Kenny halafu ikiwezekana tutoe picha zao wote wanandoa kwenye magazeti."

"Hilo wazo ninakubaliana nalo," alisema Misango na mara simu ya Mwalimu Misango ikaita.

Akiwa bado amempakata Huba ambaye sasa linyamaza, akapokea simu ambayo ilikuja bila kuonesha jina la mpigaji.

"Hallo, habari," iliuliza sauti ya kike.

"Nzuri."

"Nazungumza na Mwalimu Misango?"

"Ndiyo. Nani mwenzangu."

"Naitwa Maua, maarufu Mama Jane. Ninaishi Muhogoni, hapa jirani tu na alipokuwa akiishi Mama Kenny."

"Tunafahamiana?"

"Mimi ninakufahamu lakini nadhani wewe hunifahamu."

"Unasemaje Maua."

"Nilikuwa nina habari zinazomhusu wifi yako, Mama Kenny. Nilikuja shuleni ili tuzungumze lakini nimekuta umeshaondoka. Nimeambiwa leo umeondoka mapema ndio nikapata namba yako ya simu."

Maneno yake yalimshitua Mwalimu Misango. Akahisi mapigo ya moyo yanabadilika.

"Habari za Mama Kenny kama unazo nina hamu sana kuzisikia. Nzuri mbaya?"

"Mchanganyiko?"

Jibu hilo lilizidi kumchanganya Mwalimu Misango.

*Itaendelea*

**Nina muda mrefu simwoni na sina habari yoyote kutoka kwake. Mimi binafsi ninamtafuta sana. Ninaumwa na hajanilipa kodi miezi sita sasa... Nilidhani wewe dadake ungenisaidia kujua aliko?""Sijui alipo. Ina maana huna tetesi zozote kuhusu mahala alipo?**

# Mivutano ya kikabila yaongezeka DRC



Vijana wa DRC wakishiriki katika kampeni za uchaguzi, Bukavu, DRC.

**KINSHASA, DR Congo**

KAMISHNA wa ngazi ya juu wa Haki za Binadamu wa Umoja wa Mataifa )UN),Volker Turk, ameonya kuhusu kuongezeka kwa mivutano ya kikabila na kuzitaja ghasia za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo zinatokana na mzozo wa uchaguzi.

Uchelewesho wa hali ya juu na vurugu za urasimu, umeharibu uchaguzi wa Rais, wabunge wa taifa na majimbo pamoja na madiwani.

Mpaka sasa, Tume ya Uchaguzi imetangaza matokeo ya uchaguzi wa Rais yaliyompa ushindi mkubwa Rais aliyeko madarakani, Felix Tshisekedi.

Hata hivyo, matokeo upinzani umeyakataa matokeo hayo kwa madai kwamba ni ya udanganyifu.

"Nina wasiwasi mkubwa wa kuzuka kwa matamshi ya chuki za kikabila na uchochezi wa ghasia huko Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Congo," (DRC) alsema kamishna huyo wa UN.

Alisema wito wa ghasia uliotolewa baada ya uchaguzi, ulikuwa una mashaka hususani na maeneo ya Kivu Kaskazini na Kusini ambayo yamekubwa na makundi ya watu wenye silaha na mauaji ya kikabila ikiwemo Mikoa ya Kasai na Katanga.

Tshisekedi anatokea Kasai na Moise Katumba mmoja wa wapinzani wake wakuu, anatokea Katanga.

VOA.

## 2023 uliongoza raia kufa, kujeruhiwa kwa vilipuzi

**LONDON, Uingereza**

MWAKA 2023, ulishuhudia idadi kubwa zaidi ya majeruhi wa raia waliouawa au kujeruhiwa na vilipuzi katika zaidi ya muongo mmoja, kulingana na utafiti mpya.

Shirika la kutoa misaada kuhusu Vurugu za Kivita (AOAV) lenye makao yake makuu nchini Uingereza (AOAV), lilirekodi ongezeko la asilimia 122 la vifo vya raia vilivyosababishwa na vilipuzi mwaka jana.

Kupanda huko kumechangiwa zaidi na vita vinavyopiganwa kati ya Israel na Hamas huko Gaza na migogoro ya Ukraine, Sudan, Myanmar na Somalia.

Utafiti wa shirika la hisani lenye makao yake London unatumiwa na majukwaa ya kimataifa kama vile UN. Pia imewasilisha ushahidi wake kwa Bunge la Uingereza.

Mwaka jana, AOAV iligundua takriban matukio 7,307 ya milipuko kote ulimwenguni, kutoka 4,322 yaliyorekodiwa mwaka uliopita.

Mashambulizi hayo yalisababisha vifo vya takriban raia 15,305, na hivyo kuchangia kuongezeka kwa asilimia 122 kutoka 2022. Makumi ya maelfu ya wengine walijeruhiwa.

AOAV inaelezea vita vya Israel huko Gaza kama sababu kubwa ya ongezeko kubwa kama hilo la vifo vya raia, ikichukua karibu theluthi moja ya jumla ya ulimwengu.

Ilirekodi matukio 920 ya matumizi ya silaha za milipuko huko Gaza na kusababisha watu 9,334 kuuawa. Hiyo ni chini kuliko makadirio mengine.

BBC.

> Utafiti wa shirika la hisani lenye makao yake London unatumiwa na majukwaa ya kimataifa kama vile UN.

## Afisa wa Jeshi jela kwa ujasusi

**WASHINGTON, Marekani**

AFISA wa Jeshi la Wanamaji wa Marekani aliyekiri kutoa taarifa nyeti za kijeshi kwa China, amefungwa jela kwa zaidi ya miaka miwili.

Wenheng Zhao (26) alikiri hatia Oktoba, mwaka jana kwa kupeana taarifa kwa majasusi wa China kwa rushwa.

Zhao alikuwa afisa mdogo anayefanya kazi katika kituo cha wanamaji cha California.

Alipitisha habari kuhusu mazoezi ya kijeshi, maagizo ya operesheni na miundombinu muhimu kuanzia mwaka 2021 hadi mwaka 2023, maafisa wa Amerika walisema.

Ilielezwa kuwa afisa huyo wa jeshi, alitoa taarifa kuhusu mazoezi makubwa ya Jeshi la Wanamaji la Marekani katika eneo la Indo-Pacific, pamoja na michoro ya umeme na michoro ya mfumo wa rada ulioko kwenye kambi ya Marekani kwenye kisiwa cha Japan cha Okinawa.

Kambi ya Jeshi la Wanamaji la Marekani huko Okinawa, ni muhimu kwa shughuli zake barani Asia.

# Mtoto wa Rais Bazoum aachiwa huru kwa muda

**NIAMEY, Niger**

UTAWALA wa kijeshi nchini Niger,umemuachia huru mtoto wa Rais aliyepinduliwa madarakani Mohamed Bazoum.

Kulingana na mahakama ya Kijeshi mjini Niamey, Salem Bazoum mwenye umri wa miaka 22 ameachiwa kwa muda Jumatatu jioni na atatakiwa kuwasili mahakamani ikiwa atahitajika.

Chanzo kilicho karibu na rais Bazoum kimeliambia Shirika la Habari la AFP kwamba Salem Bazoum ameondoka Niamey kuelekea Lome, Mji Mkuu wa Togo, ambako aliwasili juzi jioni.

Togo ni miongoni mwa mataifa kadhaa ya Afrika Magharibi ambayo yamehusika katika upatanishi na utawala wa kijeshi wa Niger. Licha ya vikwazo mbalimbali, Togo imeendelea kuwa na uhusiano wa karibu na Niger.

Kulingana na televisheni ya umma ya Niger, siku ya Jumatatu iliyopita, Waziri wa Mambo ya Nje wa Togo, Robert Dussey alikuwa ziarani mjini Niamey, ambako alikutana na Waziri Mkuu.



Rais aliyepinduliwa madarakani nchini Niger Mohamed Bazoum(kulia), akisalimiana na Rais wa Ufaransa Emmanuel Macron katika Ikulu ya Elysée mjini Paris.

# Niger yaimarisha mahusiano na majirani zake

**NIAMEY, Niger**

TANGU mapinduzi ya Julai 26 mwaka jana, Niger inatawaliwa na viopngozi wa jeshi na Rais Bazoum na familia yake wanaendelea kuzuiliwa katika makazi ya rais.

Soma pia: Mawakili wa Bazoum wakanusha madai kwamba alijaribu kutoroka

Mapinduzi hayo yalilaaniwa kimataifa huku taifa hilo likikabiliwa na matatizo ya kiuchumi kufuatia vikwazo vya Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi (Ecowas).

Bei ya vyakula imepanda na kumeshuhudiwa uhaba wa bidhaa muhimu kama vile dawa, katika moja ya nchi maskini zaidi duniani.

Lakini mtawala wa kijeshi Jenerali Abdourahamane Tiani, alisema ataongoza serikali ya mpito kwa muda wa miaka mitatu kabla ya kurejesha serikali ya kiraia.

Utawala mpya wa kijeshi nchini Nige,r umejitenga na washirika wake wa jadi wa mataifa ya Magharibi hasa Ufarans na umekuwa na mahusiano ya karibu na majirani zake wawili, ambao ni Mali na Burkina Faso, ambazo pia kwa sasa zinaongozwa na wanajeshi baada ya mapinduzi.

Wanajeshi wa mwisho wa Ufaransa waliondoka Niger Desemba, mwaka jana. Kama ilivyo kwa nchi jirani za Burkina Faso na Mali, Niger inakabiliwa pia na uasi wa makundi ya kigaidi hasa katika eneo ambalo nchi hizo tatu za Sahel zinapakana.

Mwezi uliopita, Rais wa Benin, Patrice Talon, alitoa wito wa kuanzishwa upya na kwa haraka uhusiano kati ya nchi yake na nchi jirani ya Niger.

Wiki moja baadaye, Benin iliondoa vikwazo kwa bidhaa zilizoagizwa kutoka nje zinazopitia Niger kupitia Bandari ya Cotonou baada ya miezi mitano ya vikwazo.

Kwa sasa uanachama wa Niger bado umesimamishwa katika Jumuiya ya Ecowas ambayo inasema kuachiliwa kwa Bazoum na kurejea kwake madarakani, ni miongoni mwa masharti ya kulegezewa vikwazo.

Maafisa kadhaa wa serikali iliyopinduliwa wamekamatwa na wengine wamelazimika kwenda uhamishoni.

Aliyekuwa Waziri wa Nishati, Ibrahim Yacoubou, alikamatwa wiki iliyopita aliporejea nchini humo.

DW.



Mtawala wa kijeshi wa Niger, Jenerali Abdourahamane Tiani, akilihutubia taifa Julai 28,2023 siku mbili baada ya mapinduzi.

# Hawa ndio waliofungua njia za Waafrika katika michezo



Peter Ndlovu


Larbi Benbarek

Na Valensi Mbaga

Toka zamani michezo mingi ilitawaliwa zaidi na wachezaji wa Uropa na mabara mengine. Lakini, tusisahau mchango mkubwa kutoka kwa bara la Afrika. Kwa miaka mingi, Afrika imeipa soka la dunia wachezaji mashuhuri, ambao wamezalisha ufanisi kwa vilabu na nchi zao. Soka la Afrika limejawa na vipaji vingi ambavyo vitakumbukwa muda wote.

Hebu tuwatazame wanamichezo watano bora zaidi wa Kiafrika ambao wamehamasisha mamilioni kutoka kote ulimwenguni kupenda namna ya uchezaji wao na pia kuwahamasisha vijana wa kiafrika kujihusisha katika michezo hiyo

**1. Peter Ndlovu**

Peter Ndlovu aliyezaliwa 25 Februari 1973 ni kocha wa kandanda wa Zimbabwe na mchezaji wa zamani wa kulipwa ambaye aliwahi kuwa meneja wa timu ya Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini.

Peter Ndlovu ndie mchezaji wa kwanza kuwahi kucheza katika ligi kuu ya nchini Uingereza.

Kama mchezaji alikuwa mshambuliaji kutoka 1988 hadi 2011, haswa akitumia wakati huko England katika Ligi ya kuu ya EPL akianza kuwa na Coventry City na vile vile Birmingham City, Huddersfield Town, na Sheffield United.

Muda uliobaki wa maisha yake aliutumia katika bara lake la asili yani Afrika akiwa na Highlanders, Mamelodi Sundowns, Thanda Royal Zulu, Highfield United na Black Mambas. Alicheza mechi 81 kwa nchi yake, akifunga mabao 37.

Tangu kustaafu, Ndlovu amehamia uwalimu wa soka na amefanya kazi kama meneja msaidizi wa Zimbabwe.

**2. Larbi Benbarek**


Labri Benbarek almaarufu pia kama Ben Barek au Ben M'barek. Mwamba huyu alizaliwa Juni 16,1917huko Cassablanca Morocco wakati huo Morroco ilikuwa sehemu ya Ufaransa. Kutokana na uchezaji wake Alipata jina la utani la "Black Pearl" na anachukuliwa kuwa mmoja wa wachezaji bora wa soka wa wakati wake.

Ben Barek alianzisha kampeni ya Ligi ya Uropa, na haswa ya Ufaransa na Uhispania, kwa wachezaji wazaliwa wa Kiafrika. Alifika Marseille, Ufaransa, akiwa na umri wa miaka 20 na akawa kipenzi cha mashabiki papo hapo kwa ustadi wake na uwezo wake wa kiufundi. Anakumbukwa sana kama mwanasoka wa kwanza wa Kiafrika aliyefanikiwa barani Ulaya. Kazi yake ilikatizwa na kuanza kwa Vita vya dunia ya pili, lakini badae alirudi kwenye ubora wake akiwa na Stade Français FC, hatimaye akahamia Uhispania na Atlético Madrid, ambapo sifa yake ya kimataifa ilienea. Jina lake la utani na mashabiki nchini Uhispania lilikuwa "Mguu wa Mungu". Kwa usaidizi wa Benbarek, Atlético ilishinda La Liga mwaka wa 1950 na 1951.

**3.Dikembe Mutombo**

Dikembe Mutombo Mpolondo Mukamba Jean-Jacques Wamutombo amezaliwa 25 Juni 1966 ni Mmarekani mwenye asili ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo mchezaji

>>Inaendelea uk. 21



Dikembe Mutombo

# Hawa ndio waliofungua njia za Waafrika katika michezo



François Zahoui

>>Inatoka uk. 20

mstaafu wa mpira wa kikapu. Mutombo alicheza misimu 18 katika chama cha mpira wa kikapu cha kitaifa (NBA).

Dikembe Mutombo Denver Nuggets Alianza kazi yake na Georgetown Hoyas ya mpira wa kikapu, kwa kawaida kama mmoja wa wachezaji anayetetea wakati wote. Alishinda tuzo ya mchezaji na mkabaji kwa mwaka mara nne, pia aliweza kufuzu mara nane katika timu ya wachezaji mastaa

Mutombo alitangaza kustaafu. Tarehe 11 Septemba 2015 aliingizwa kwenye ukumbi wa umaarufu wa mpira wa kikapu wa Naismith. Na alisimama kama mwafrika wa kwanza kufungua njia ya mchezo huu kwa waafrika wengine.

**4.François Zahoui**


Francois Zahoui amezaliwa 21 Julai 1961 ni mchezaji na meneja wa zamani wa soka wa Ivory Coast ambaye anasimamia timu ya taifa ya Jamhuri ya Afrika ya Kati. Alikuwa mwanasoka wa kwanza Mwafrika kucheza Serie A.Na kutokana na mafanikio yake ilikuwa moja ya chachu kubwa kwa vijana wa kiafrika kuanza kuamini katika soka la kulipwa na baadae kuanza kunufaika nalo.

Mnamo 2010, Zahoui alichaguliwa kuchukua nafasi ya Sven-Goran Eriksson kama kocha mkuu wa timu ya taifa ya Ivory Coast. Mnamo 2015, aliteuliwa kama mkufunzi mkuu wa Niger, akiondoka mnamo Septemba 2019.Wiki moja baadaye akawa meneja wa Jamhuri ya Afrika ya Kati.

**5.George Weah**

George Manneh Oppong Weah aliyezaliwa 1 Oktoba 1966 ni mwanasiasa wa Liberia na mwanasoka wa zamani ambaye ni rais anayemaliza muda wake wa Liberia, akihudumu ofisini kati ya 2018 na 2024.

Alicheza kama mshambuliaji katika maisha yake ya soka la kulipwa kwa miaka 18, ambayo lilimalizika mwaka wa 2003. Weah ni mwanasoka wa kwanza wa zamani wa kulipwa kuwa mkuu wa nchi.



George Weah

Baada ya kuanza maisha yake ya soka nchini Liberia, Weah alitumia miaka 14 kuchezea klabu za Ufaransa, Italia na Uingereza.



Arsène Wenger alimleta Ulaya kwa mara ya kwanza, na kumsajili kwa Monaco mwaka 1988. Weah alihamia Paris Saint-Germain mwaka 1992 ambapo walishinda Division 1 mwaka 1994 na kuwa mfungaji bora wa UEFA Champions League 1994-95.

Baadae alisajiliwa na AC Milan mwaka 1995 ambapo alitumia misimu minne yenye mafanikio, akishinda Serie A mara mbili na akahamia Ligi ya kuu ya Uingereza kuelekea mwisho wa maisha yake ya soka na aliwahi kucheza Chelsea na Manchester City, akishinda Kombe la FA akiwa na kikosi cha kwanza, kabla ya kurejea Ufaransa kuichezea Marseille mwaka wa 2001.

Alimaliza soka lake akiwa na Al Jazira mwaka wa 2003. Pamoja na yote Weah alikuwa mmoja wa wachezaji bora ambao hawakuwahi kushinda UEFA Champions League.

Hao ni baadhi ya magwiji wa enzi hizo kwenye michezo katika bara la Africa ambao walikuwa chanzo cha imani kwa wengine katika nyenzo ya kimichezo.

kwa sasa Africa ni moja kati ya mabara bora katika michezo na ushiriki wa wanamichezo kutoka Afrika umeongezeka kwa kiasi kikubwa. Huwezi kushangaa kumuona mwafrika akicheza NBA, EPL, Seria A, Eredivise,Laliga au ligi yeyote kubwa barani ulaya kwani vijana wakiafrika wamezidi kuonyesha viwango vikubwa na kuzidi kukuza thamani zao na Africa kwa ujumla.

# Ni makocha au uongozi mbovu?

**Na Valensi Mbaga**

KIPINDI cha hivi karibuni imekuwa kitu cha kawaida katika Ligi yetu kusikia kocha fulani kafukuzwa kuifundisha timu kutokana na kiwango kibovu cha uchezaji na kushindwa kupata matokeo katika timu husika.

Lakini tukirudi nyuma katika historia ya soka makocha wengi waliofanya vizuri kama Sir Alex Ferguson, Jose Mourinho , Arsen Wenger alivyoifua Arsenal, Pep Guardiola na Manchester city yake, Thomas Tuchel na ile Chelsea iliyobeba hadi Uefa, Wote hawa walipata muda wa kuwa na timu kwa miongo miwili au zaidi na kufanikiwa kutengeneza timu bora zaidi katika soka. Lakini katika soka la kwetu timu nyingi haziwapi makocha muda wa kutengeneza timu na badala yake wakishindwa kufanya vizuri wanafukuzwa. Swali ni je? Makocha ndio hawana uwezo wa kufundisha timu au ubora wa wachezaji au ni uongozi wa tiimu ndio unakwamisha mafanikio ya timu.





**1: Mecky Mexime**

Mexime ni moja kati ya makocha wakubwa katika nchi yetu na ni mzoefu kwa ngazi ya klabu na ngazi ya Taifa .Akitokea Kagera Sugar ambapo aliondoka kutokana na kiwango kibovu kwa kuiongoza Kagera Sugar katika michezo 13 na kuipa ushindi katika michezo mitatu kutoa sare mchezo minne na kupoteza michezo sita. Na kutokana na kiwango hiki kimepelekea walima sukari hao kutokea kagera kushika nafasi ya 14 wakiwa na alama 13.

Kwa sasa Mexime anawaongoza wana mbogo maji Ihefu Sc ambapo ametambulishwa kama kocha mpya kufua tmu hyo.



**2: Mwynyi Zahera**

Mkongwe Mwynyi Zahera aliyewahi kuwa kocha wa Yanga Sc, Polisi Tanzania na Coastal Union ambae kwa sasa ametambulishwa na wauaji wa kusini Namungo Sc ni moja kati ya magwiji wa soka la ndani. Zahera aliondoka kwa Wagosi wa kaya kutokana na kukosa muendelezo mzuri wa matokeo na kuwaweka pazuri wanamangushi.

Coastal union chini ya Mwyinyi Zahera waliambulia alama tisa tu kabla ya kuondoka kwa kocha huyo na kwa sasa wamefanikiwa kupata alama 19 katika michezo 14 na kujiweka katika nafasi ya sita nyuma ya Singida FG kwa tofauti ya alama moja.

**3: Zuberi Katwila**

Kocha huyu ambae kwa sasa amerudi Nyumbani kwake kisoka na yuko na mapambano mazito ndani ya Mtibwa Sugar ya kuondoka mkiani ni moja kati ya walimu wazuri ambao wamekuwa wakifanya vizuri katika soka la Tanzania.

Katwila amekuwa na wakati mgumu sana na akiifundisha Ihefu Sc aliambulia matokeo mabovu baada ya ushindi dhidi ya Yanga Sc na baada ya hapo alipitia wakati mgumu na kupoteza michezo mingi na kwake sare ndo ilikuwa ushindi. Hali hio ilipelekea Katwila kuachana na Wana mbogo maji hao kutoka mbarali na kurudi katika timu yake aliyowahi kuichezea Mtibwa sugar

Hao ni baadhi ya wakongwe ambao mpaka sasa bado wanahangaika kupata timu za kufundisha kwa muda mrefu. Na swali linabaki kwao je? ni nini wafanye ili kupata wanachostahili kwenye timu wanazofundisha. Na je uongozi unatoa mchango unaohtajika kwao ili wao kufanya vizuri na kupata matokeo.

Tukirudi katika kuangalia soka la kisasa linahitaji utulivu wa timu. Kocha anahitaji kuwajua na kuzoea zaidi wachezaji wake na kutengeneza mfumo maalumu ambao utawapa matokeo mazuri wakati wote. Na kwa Tanzania Yanga Sc ni moja ya timu zilizoonyesha kutulia na kuamini mipango ya muda mrefu ya waalimu na hali hii kuonekana kuwalipa na kupelekea kutengeneza kikosi imara na chenye muunganiko mzuri na uliowapa mafanikio makubwa.

> **Je? ni nini wafanye ili kupata wanachostahili kwenye timu wanazofundisha. Na je? Uongozi unatoa mchango unaohtajika kwao ili wao kufanya vizuri na kupata matokeo.**





# Kona ya Urembo

Na Hidaya Machuppa
Simu: +255 765 828 219



# Pendeza na urembo wa Henna






HENNA, jina la Kiajemi la Lawsonia inermis, shrub ya jangwa yenye maua ambayo hutoa rangi nyekundu. Mara mbili kwa mwaka majani ya hina huvunwa, kukaushwa, na kusagwa kuwa unga mwembamba. Kwa zaidi ya miaka 9,000 henna imetumika kwa rangi ya nywele nyekundu na kwa sanaa ya mehndi.

Henna ina asidi ya hennotannic, rangi inayounganisha na collagen katika seli za ngozi na keratini ya vidole na nywele, na kuacha nyuma ya rangi nyekundu-kahawia.

Henna ni vipodozi vya zamani zaidi vilivyoandikwa na ni laini na baridi kwenye ngozi. Inapunguza uchovu wa joto na hata ni kizuizi cha jua cha asili. asili ya Henna ni Asia na pwani ya Mediterania ya Afrika na sasa inastawi katika hali ya hewa ya joto duniani kote.





**Viungo**

Unga wa asili wa hina unaopatikana na tunachanganya kwa mkono unga huo na majani ya kusaga ya hina, maji ya limao, na mafuta muhimu ya daraja la kunukia yenye harufu nzuri.

**Hudumu kwa Muda Gani?**

Miundo huchukua muda wa siku 7-10, kulingana na kemia ya mwili, muda gani kuweka iliruhusiwa kuingia ndani, na eneo kwenye mwili. Inadumu kwa muda mrefu zaidi kwenye mikono na miguu, inafifia haraka zaidi kwenye mikono, kifua na mgongoni ambapo ngozi ni nyembamba. Rangi itakuwa ya rangi ya chungwa hafifu mwanzoni na kuzama hadi nyekundu-kahawia wakati wa saa 48 zinazofuata, na kufifia polepole ngozi yako inapochanua.

**Inaumiza?**

Hapana, hina inahisi kama losheni na inapoa. Upakaji wa henna unaweza kustarehesha na kufurahisha sana, haswa katika miezi ya joto ya kiangazi kwani inapoa na kulainisha ngozi

**Je, ni salama?**

Mmea wa hina ni moja ya vipodozi vya zamani zaidi kuwahi kutumika na ni salama sana.

Henna nyekundu ya asili, inapotumiwa kwenye ngozi mara chache husababisha athari mbaya, ikiwa una wasiwasi unapaswa kufanya mtihani mdogo wa kiraka kwanza. Henna asilia ni salama hata kwa watoto kwani haina dyes za kemikali hatari au viambajengo vikali.

**Rangi Gani?**

Doa nyekundu-kahawia itatofautiana katika giza na kemia ya mwili wa kila mtu, eneo la mwili lililochaguliwa, na urefu wa muda wa kuweka kwenye ngozi.

**Sio Nyeusi Kamwe**

'Henna nyeusi' hutengenezwa kwa kutumia rangi yenye kemikali yenye sumu ambayo inaweza kusababisha makovu ya kudumu na ndani kuharibu figo, ini na malengelenge kwenye ngozi.

**Matumizi ya henna Viwanda**

Henna imetumika sana katika utengenezaji wa bidhaa za ngozi. Inatumika kupamba ngozi za ngoma, kufa kwa jumla kwa ngozi na kwa nguo za kuchorea. Ilitumiwa na Waajemi kupaka rangi kwato na manes ya farasi wao. Waajemi walipoivamia India wakiwa wamepanda farasi karibu 712 CE, walileta Uislamu na Mehndi. Henna kwa hakika ilitumiwa nchini India kabla ya wakati huu lakini si kwa matumizi yaliyoenea, maarufu ambayo yalikuzwa chini ya utawala wa Kiislamu.

**Hutumika kama dawa.**

Mmea wa henna umetumika kwa madhumuni ya dawa kwa karne nyingi. Moja ya mali yake kuu ni ya wakala



wa baridi. Ni kwa sababu hii kwamba henna hutumiwa kwa kuchomwa moto na scrapes na mara nyingi hutumiwa kutibu uchovu wa joto na kuleta homa ya mtu mgonjwa.

Inaweza pia kutumika kwa ngozi kutibu aina mbalimbali za vipele ikiwa ni pamoja na mguu wa wanariadha na wadudu. Henna hutoa kinga kamili ya jua, jaribu kuoka ngozi na mehndi yako.

**Uzuri.**

Henna imetumika katika mila na desturi za urembo tangu nyakati za zamani. Ni kipodozi kongwe zaidi kilichorekodiwa na kinatumika sana katika Mashariki ya Kati na ya Mbali. Inatumika kwa mali yake ya unyevu na kulinda jua pamoja na rangi ya nywele, na uwezo wake wa kubadilisha ngozi na mifumo nyekundu.

Inasemekana kwamba Cleopatra na Nefertiti walitumia hina pamoja na Fatima, bintiye Mtume Muhammad, na Mumtaz Mahal, ambapo Taj Mahal ilijengwa Wakati & Kwa nini Inatumika

**Mila ya Ndoa ya Kimila ya Mashariki**

Harusi ni matumizi kuu ya mapambo ya mikono na miguu ya bibi arusi kabla ya sherehe ya ndoa katika tamaduni za Kihindu na Kiislamu. Mehndi ya jadi ya harusi inaweza kuwa mnene sana, inayofanana na glavu za lace. Mara nyingi hufunika sehemu za juu na viganja vya mikono inayopanua mikono, na sehemu za juu za miguu zinaenea hadi vifundoni na miguu. Mehndi ya harusi ni ishara ya hali na sherehe na ni moja ya zawadi za kwanza kutoka kwa mume hadi mke.

**Mimba na Matukio Mengine**

Sherehe za kila aina ni pamoja na mehndi kwani inachukuliwa kuepusha maovu, kulinda dhidi ya jicho baya, kutoa bahati nzuri na kwa ujumla kuwa ya kupendeza kwa asili kwa sababu ya rangi nyekundu. Inaweza kujumuishwa katika siku za kuzaliwa, sherehe za kutaja majina, siku za kuzaliwa, bar mitzvahs, Diwali, Ramadhani na sikukuu nyingine nyingi za kidini, sherehe na mila za kitamaduni.

Utumiaji wa hina na karamu inayolingana kwa kawaida huwa ni ya wanawake pekee. Mara nyingi wanafamilia wa kike na marafiki wa karibu wa kike watashiriki, hii inaunda fursa ya kupokea msaada na ushauri. Ni wakati ambapo wanawake, haswa wale walio katika nyumba ya wanawake wanaweza kujitenga na sheria za muundo wa maisha yao na kupumzika.

Leo yetu ndiyo kesho yetu

Uelekeo Spoti

| Jumatano Januari 10 - 16, 2024 |

## Ni mechi ya kisasi, heshima

Na Mwandishi Wetu

JE, Vijana wa wa Mzee wa Kapelo, Abdelhak Benchikha watakaoibuka na kicheko Leo au ni wazee wa kutimua timua watakaocheka mwisho?

Singida haijawahi kufunga Simba ambapo ushindi wake mkubwa ni sare. Katika michuano ya Mapinduzi Singida ilikula kisago na inahitaji kushinda mechi ya leo kuweza kugeuza uteja na kuwa heshima.

Simba inayojijenga upya inahitaji kuthibitisha ubora sasa na kushinda mchezo wa Jumatano ili kutafuta Kombe hilo na kuongeza taji la pili klabuni kwao baada ya Ile Ngao ya Hisani iliyotwaa Tanga mbele ya Yanga.






# Tumalize Ubishi

Na Mwandishi Wetu

MICHUANO ya Kombe la Mapinduzi imeibua nongwa kwa vigogo wa soka nchini timu za Simba na Yanga.

Nongwa hiyo inatokana na hatua ya timu za Yanga na Azam kutolewa kwenye mashindano hayo katika hatua ya robo fainali.

Yanga alipigwa mara 3-1 na APR ya Rwanda ambayo katika hatua ya makundi walitoka sare ya bila kufungana na Simba. APR ilishika nafasi ya tatu katika kundi la Simba nyuma ya Singida.

Azam ilitolewa robo fainali na Singida kwa mabao 2-1. Matokeo hayo ndio ambayo Simba iliyapata kutoka kwa Singida.

NONGWA: Simba kupitia kwa Ofisa Habari wao, Ahmed Ally wametoa ombi michuano ijayo timu hizo tatu za Bara ziwekwe kundi moja.

"Kuna timu zinajifungisha makusudi ili kukimbia, cha msingi wote tuwekwe kundi moja ili tumalizane,* alisema.

Kauli hiyo iliwachefua Yanga ambapo walitoa Kauli kupitia kwa Makamu wa Rais wao, Arafat Haji na Meneja Uhusiano Ally Kamwe.

Haji alisema timu yake iko tayari kwa maana inataka kusimika mabango mengine baada ya yale ya awali ya 1-5.

Kamwe akaongeza endapo Simba wanajiamini waandike barua kuomba mechi.



# Yanga yarudisha ofisi Jangwani

Na Michael Maurus

BAADA ya kuendesha shughuli zake katika jengo la GSM maarufu kama Salamander zamani, Uongozi wa klabu ya Yanga umeamua kurudi Makao Makuu ya klabu hiyo mitaa ya Twiga na Jangwani.

Kwa takribani miaka miwili sasa Yanga hawakuwa wakitumia jengo lao kazi za Utawala bali walihamia Posta katika jengo la mfadhili wao mkuu.

Tumefanya maboresho makubwa na ya kisasa kwenye jengo letu la Jangwani.




Mungu akijalia mwishoni mwezi huu tutakuwa na jengo bora na la kisasa ambapo ofisi na shughuli zote za Klabu zitafanyika pale," alisema Rais wa Yanga, Mhandisi Hersi Said.

Kiongozi huyo alisema klabu yao imefanya maboresho pia katika mfumo wa utendaji kati ya kampuni na klabu ambapo Taasisi hizi zitakuwa na Mahusiano ya kibiashara.

"Tunajenga mfumo ambao mwekezaji akija anakuta muundo bora wa utawala, kimapato. Malengo yetu ni kuhakikisha kuwa na timu imara kiuchumi

Alisema ili kulinda maslahi ya Klabu wamehakikisha kinachopelekwa kwenye kampuni ni nembo na biashara ya timu na kwamba mali zote za Yanga zitabaki kuwa mali ya Yanga na sio mali ya kampuni.

Alisema Kampuni mpya ya Yanga haitaimiliki Yanga, bali Yanga ndio itamiliki kampuni.

"Mwekezaji hana haki na mali za klabu kama vile uwanja na majengo," alisema.